# Kumbukumbu La Torati

*Amri Ya Kuondoka Mlima Horebu*

1 Haya ni maneno Mose aliyoyasema kwa Israeli yote jangwani mashariki ya Yordani, ambayo iko Araba, inayokabiliana na Sufu, kati ya Parani na Tofeli, Labani, Haserothi na Dizahabu.
2 (Ni mwendo wa siku kumi na moja kutoka Horebu kwa njia ya Mlima Seiri mpaka Kadesh-Barnea.)
3 Katika mwaka wa arobaini, siku ya kwanza ya mwezi wa kumi na moja, Mose aliwatangazia Waisraeli yale yote BWANA aliyomwamuru kuwahusu.
4 Hii ilikuwa baada ya kumshinda Sihoni mfalme wa Waamori, ambaye alitawala Heshboni, na pia huko Edrei alikuwa amemshinda Ogu mfalme wa Bashani, ambaye alitawala huko Ashtarothi.
5 Huko mashariki ya Yordani katika nchi ya Moabu, Mose alianza kuielezea sheria hii, akisema:

6 BWANA Mungu wetu alisema nasi huko Horebu, "Mmekaa vya kutosha katika mlima huu.
7 Vunjeni kambi, msonge mbele kuelekea nchi ya vilima ya Waamori; nendeni kwa watu wote ambao ni majirani wa Araba, katika milima, upande wa magharibi chini ya vilima, katika Negebu na kandokando ya pwani, mpaka nchi

ya Wakanaani hadi Lebanoni, na kufika mto mkubwa Frati.
8 Tazama, nimewapa ninyi nchi hii. Ingieni mkaimiliki nchi ambayo BWANA aliapa kuwa angaliwapa baba zenu, Abrahamu, Isaki na Yakobo, pamoja na vizazi vyao baada yao."

### *Uteuzi Wa Viongozi (Kutoka 18:13-27)*

9 Wakati ule niliwaambia, "Ninyi mmekuwa mzigo mzito sana kwangu kuwachukua peke yangu.
10 BWANA Mungu wenu ameongeza hesabu yenu, hivi kwamba leo ninyi ni wengi kama nyota za angani.
11 Naye BWANA, Mungu wa baba zenu na awaongeze mara elfu na kuwabariki kama alivyoahidi!
12 Lakini mimi nitawezaje kubeba matatizo yenu, na mizigo yenu, na magomvi yenu peke yangu?
13 Chagueni baadhi ya watu wenye hekima, wenye ufahamu na wanaoheshimika kutoka kila kabila lenu, nami nitawaweka juu yenu."
14 Mlinijibu, "Shauri ulilolitoa ni zuri."
15 Kwa hiyo niliwachukua wanaume viongozi wa makabila yenu, wenye hekima na wanaoheshimika, nami nikawateua wawe na mamlaka juu yenu kama majemadari wa maelfu, wa mamia, wa hamsini, na wa makumi, na kama maafisa wa makabila.
16 Nami wakati ule nikawaagiza waamuzi wenu: Sikilizeni magomvi kati ya ndugu zenu na mwamue kwa haki, hata kama shauri ni kati ya

ndugu wa Kiisraeli, au kati ya mmoja wa ndugu
wa Kiisraeli na mgeni.
17 Msionyeshe upendeleo katika maamuzi;
wasikilizeni wote sawasawa, wadogo kwa
wakubwa. Msimwogope mtu yeyote, kwa
kuwa hukumu ni ya Mungu. Mniletee mimi
shauri lolote lililo gumu sana kwenu, nami
nitalisikiliza.
18 Nami wakati ule niliwaambia kila kitu am-
bacho mngefanya.

### *Wapelelezi Wanatumwa (Hesabu 13:1-33)*

19 Kisha, kama BWANA Mungu wetu alivyotu-
amuru, tuliondoka kutoka Horebu na kwenda
kuelekea nchi ya vilima ya Waamori, kupitia
jangwa lile kubwa lote la kutisha, lile mliloliona,
nasi tukafika Kadesh-Barnea.
20 Kisha niliwaambia, “Mmefika katika nchi ya
vilima ya Waamori, ambayo BWANA Mungu wetu
anatupa.
21 Tazama, BWANA Mungu wenu amewapa
nchi. Pandeni mkaimiliki kama BWANA, Mungu
wa baba zenu, alivyowaambia. Msiogope, wala
msikate tamaa.”
22 Ndipo ninyi nyote mkanijia na kusema,
“Tupeleke watu watutangulie kuipeleleza nchi
kwa ajili yetu, na kutuletea taarifa kuhusu njia
tutakayopita, na miji tutakayoiendea.”
23 Wazo hilo lilionekana zuri kwangu; kwa
hiyo niliwachagua watu wenu kumi na wawili,
mwanaume mmoja kutoka kila kabila.

24 Waliondoka na kukwea katika nchi ya
vilima, wakafika katika Bonde la Eshkoli na
kuipeleleza.
25 Wakachukua baadhi ya matunda ya nchi,
wakatuletea na kutuarifu, "Ni nchi nzuri am-
bayo BWANA Mungu wetu anatupa."

### *Uasi Dhidi Ya BWANA*
### *(Hesabu 14:20-45)*

26 Lakini hamkuwa tayari kukwea, mkaasi
dhidi ya amri ya BWANA Mungu wenu.
27 Mkanung'unika ndani ya mahema yenu na
kusema, "BWANA anatuchukia, kwa hiyo alitutoa
Misri ili kututia mikononi mwa Waamori ku-
tuangamiza.
28 Twende wapi? Ndugu zetu wametufanya
kufa moyo. Wanasema, 'Watu wa huko wana
nguvu zaidi na ni warefu kuliko sisi tulivyo; miji
ni mikubwa, yenye kuta zilizofika juu angani.
Zaidi ya hayo, tumewaona Waanaki huko.' "
29 Ndipo nikawaambia, "Msihofu, wala msi-
waogope.
30 BWANA Mungu wenu anayewatangulia,
atawapigania, kama alivyofanya kwa ajili yenu
huko Misri, mbele ya macho yenu hasa,
31 na pia huko jangwani. Huko mliona jinsi
BWANA Mungu wenu alivyowachukua, kama
baba amchukuavyo mwanawe, katika njia yote
mliyoiendea mpaka mkafika mahali hapa."
32 Pamoja na hili, hamkumtegemea BWANA
Mungu wenu,
33 ambaye aliwatangulia katika safari yenu,
kwa moto usiku na kwa wingu mchana,

kuwatafutia mahali penu pa kupiga kambi na kuwaonyesha njia mtakayoiendea.

34 Wakati BWANA aliposikia lile mlilosema, alikasirika, akaapa, akasema:

35 "Hakuna mtu wa kizazi hiki kiovu atakayeona nchi nzuri niliyoapa kuwapa baba zenu,

36 isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune. Yeye ataiona, nami nitampa yeye na wazao wake nchi aliyoikanyaga kwa miguu, kwa sababu alimfuata BWANA kwa moyo wote."

37 Kwa sababu yenu BWANA pia alinikasirikia mimi, akasema, "Hutaingia hiyo nchi pia.

38 Lakini msaidizi wako, Yoshua mwana wa Nuni, ataingia. Mtie moyo, kwa sababu atawaongoza Waisraeli kuirithi hiyo nchi.

39 Wale watoto ambao mliwasema wangelichukuliwa mateka, yaani watoto wenu ambao bado hawajui jema na baya, wataingia katika nchi. Nitawapa hiyo nchi, nao wataimiliki.

40 Bali ninyi geukeni, mwondoke kuelekea jangwani kwa kufuata njia ya Bahari ya Shamu."

41 Ndipo mkanijibu, "Tumemtenda BWANA dhambi. Tutakwenda kupigana, kama BWANA Mungu wetu alivyotuamuru." Hivyo kila mmoja wenu akachukua silaha zake, huku mkifikiri kuwa ni rahisi kukwea katika nchi ya vilima.

42 Lakini BWANA aliniambia, "Waambie, 'Msipande kupigana, kwa sababu sitakuwa pamoja nanyi. Mtashindwa na adui zenu.' "

43 Hivyo niliwaambia, lakini hamkutaka kusikia. Mliasi dhidi ya amri ya BWANA, na

katika kiburi chenu mlienda katika nchi ya
vilima.
44 Waamori ambao waliishi katika vilima hivyo
waliinuka dhidi yenu, wakawafukuza kama
kundi la nyuki wakiwapiga njia yote ya Seiri
mpaka Horma.
45 Mlirudi na kulia mbele za BWANA, lakini
Mungu hakusikiliza kilio chenu, wala hakuwa-
jali.
46 Hivyo mlikaa Kadeshi kwa siku nyingi, kwa
muda ule wote mliokaa huko.

# 2

*Kutangatanga Jangwani*

1 Kisha tukageuka nyuma na kusafiri kuelekea
jangwani kwa njia inayoelekea Bahari ya Shamu,
kama BWANA alivyonielekeza. Kwa muda mrefu
tulitembea kuzunguka vilima katika nchi ya
Seiri.
2 Kisha BWANA akaniambia,
3 "Umetembea kuzunguka hii nchi ya vilima
kwa muda wa kutosha; sasa geukia kaskazini.
4 Wape watu maagizo haya: 'Mko karibu
kupita katikati ya nchi ya ndugu zako am-
bao ni wazao wa Esau, ambao wanaishi Seiri.
Watawaogopa, lakini mwe waangalifu.
5 Msiwachokoze kwa vita kwa maana sitawapa
ninyi sehemu yoyote ya nchi yao, hata se-
hemu ya kutosha kuweka wayo wenu juu yake.
Nimempa Esau nchi ya vilima ya Seiri kama yake
mwenyewe.
6 Mtawalipa fedha kwa chakula mtakachokula
na maji mtakayokunywa.' "

7 BWANA Mungu wenu amewabariki kwa kazi
yote ya mikono yenu. Amewalinda katika safari
yenu katikati ya jangwa hili kubwa. Kwa mi-
aka hii arobaini BWANA Mungu wenu amekuwa
pamoja nanyi, na hamkupungukiwa na kitu
chochote.
8 Basi tulipita kwa ndugu zetu wazao wa Esau
ambao wanaishi Seiri. Tuligeuka kutoka njia ya
Araba ambayo inatokea Elathi na Esion-Geberi,
tukasafiri kufuata njia ya jangwa la Moabu.

9 Kisha BWANA akaniambia, “Usiwasumbue
Wamoabu kwa vita, kwa kuwa sitawapa sehemu
yoyote ya nchi yao. Nimetoa nchi ya Ari kwa
wazao wa Loti kama milki yao.”

10 (Waemi walikuwa wakiishi huko hapo za-
mani, watu wenye nguvu na wengi, warefu
kama Waanaki.
11 Kama walivyokuwa Waanaki, hao pia wa-
likuwa kama Warefai, lakini Wamoabu wali-
waita Waemi.
12 Wahori waliishi Seiri, lakini wazao wa Esau
waliwafukuza. Waliwaangamiza Wahori na
kukaa mahali pao, kama Waisraeli walivyofanya
katika nchi ambayo BWANA aliwapa kama milki
yao.)

13 BWANA akasema, “Sasa ondokeni mvuke
Bonde la Zeredi.” Hivyo tukavuka bonde.

14 Miaka thelathini na minane ilipita tangu
wakati tulipoondoka Kadesh-Barnea mpaka
tulipovuka Bonde la Zeredi. Kwa wakati huo
kile kizazi chote cha wanaume kuanzia wale
wawezao kwenda vitani kilikuwa kimekufa,
kama BWANA alivyokuwa amewaapia.

15 Mkono wa BWANA uliwakabili hadi
alipowaangamiza wote huko kambini.

16 Ikawa baada ya mtu wa mwisho kuanzia
wale wawezao kwenda vitani kufa,
17 BWANA akaniambia,
18 “Leo utapita katika nchi ya Moabu huko Ari.
19 Utakapokuja kwa Waamoni, msiwasumbue
wala kuwachokoza kwa vita, kwa kuwa sitawapa
ardhi yoyote iliyo ya Waamoni kuwa milki yenu.
Nimeitoa kama milki ya wazao wa Loti.”

20 (Hiyo pia ilidhaniwa kuwa nchi ya Warefai
waliokuwa wakiishi huko, lakini Waamoni wali-
waita Wazamzumi.
21 Walikuwa watu wenye nguvu na wengi,
warefu kama Waanaki. BWANA akawaangamiza
kutoka mbele ya Waamoni, ambao waliwa-
fukuza na kukaa mahali pao.
22 BWANA alikuwa amefanya vivyo hivyo kwa
wazao wa Esau, ambao waliishi Seiri, wakati
alipowaangamiza Wahori watoke mbele yao.
Waliwafukuza na wao wakaishi mahali pao
mpaka leo.
23 Nao Waavi ambao waliishi katika vijiji
mpaka Gaza, Wakaftori waliokuja kutoka Kaftori
waliwaangamiza na kukaa mahali pao.)

24 “Ondoka sasa na uvuke Bonde la Arnoni.
Tazama, nimemweka mikononi mwako Sihoni
Mwamori, mfalme wa Heshboni na nchi yake.
Anza kuimiliki nchi hiyo na umwingize katika
vita.
25 Siku hii ya leo nitaanza kuwatia hofu na
woga mataifa yote chini ya mbingu wawaogope

ninyi. Watakaposikia taarifa zenu, watatetemeka na kufadhaika kwa sababu yenu.”

### *Kushindwa Kwa Sihoni Mfalme Wa Heshboni (Hesabu 21:21-30)*

26 Kutoka jangwa la Kedemothi nilituma wajumbe wenye maneno ya amani kwa Sihoni mfalme wa Heshboni kusema,
27 “Turuhusu tupite katika nchi yako. Tutapita katika barabara kuu, hatutageuka kuume wala kushoto.
28 Tuuzie chakula tule na maji tunywe kwa thamani yake katika fedha. Turuhusu tu tupite kwa miguu,
29 kama wazao wa Esau ambao wanaishi Seiri na Wamoabu ambao wanaishi Ari walivyotufanyia, mpaka tuvuke Yordani kuingia nchi ambayo BWANA Mungu wetu anatupatia.”
30 Lakini Sihoni mfalme wa Heshboni alikataa kuturuhusu kupita. Kwa kuwa BWANA Mungu wako alikuwa ameifanya roho yake kuwa ngumu na moyo wake kuwa mkaidi ili amweke kwenye mikono yenu, kama alivyofanya sasa.

31 BWANA akaniambia, “Tazama, nimeanza kuwapa Mfalme Sihoni na nchi yake kwako. Sasa anzeni kuishinda na kuimiliki nchi yake.”

32 Wakati Sihoni pamoja na jeshi lake lote walipokuja kukutana nasi katika vita huko Yahazi,
33 BWANA Mungu wetu alimweka mikononi mwetu, nasi tukamwangamiza pamoja na wanawe na jeshi lake lote.

34 Kwa wakati ule tuliteka miji yake yote na
kuiangamiza kabisa: wanaume, wanawake na
watoto. Hatukumwacha yeyote.
35 Lakini mifugo na nyara tulizoziteka kutoka
ile miji tulijichukulia wenyewe.
36 Kutoka Aroeri kwenye ukingo wa Bonde la
Arnoni, kutoka mji ulio ndani ya bonde, hata
mpaka Gileadi, hapakuwa na mji hata mmoja
uliokuwa na nguvu kutushinda. BWANA Mungu
wetu alitupa yote.
37 Lakini kulingana na amri ya BWANA Mungu
wetu, hamkujiingiza katika nchi yoyote ya Waa-
moni, wala katika sehemu yoyote iliyo kan-
dokando ya Mto Yaboki, wala katika miji iliyoko
katika vilima.

# 3

### *Kushindwa Kwa Ogu Mfalme Wa Bashani (Hesabu 21:31-35)*

1 Kisha tukageuka tukakwea kufuata njia iliy-
oelekea Bashani, Ogu mfalme wa Bashani akaon-
doka na jeshi lake lote kupigana na sisi huko
Edrei.
2 BWANA akaniambia, “Usimwogope kwa kuwa
nimekwisha mkabidhi mikononi mwako pamoja
na jeshi lake lote na nchi yake. Umfanyie
sawasawa na ulivyomfanyia Sihoni mfalme wa
Waamori, ambaye alitawala huko Heshboni.”
3 Hivyo BWANA Mungu wetu pia akamweka
Ogu mfalme wa Bashani pamoja na jeshi lake
lote mikononi mwetu. Tuliwaangamiza wote,
hakubakia hata mmoja.

4 Wakati huo tuliteka miji yake yote. Hakuna
mji hata mmoja kati ya ile sitini ambao hatuku-
uteka, yaani eneo lote la Argobu, utawala wa
Mfalme Ogu katika Bashani.
5 Miji yote hii ilijengewa ngome zenye kuta
ndefu zenye malango na makomeo, pia ku-
likuwako na vijiji vingi ambavyo havikujengewa
kuta.
6 Tuliwaangamiza kabisa, kama tulivy-
omfanyia Sihoni mfalme wa Heshboni,
tukiangamiza kila mji, yaani wanaume,
wanawake na watoto.
7 Lakini wanyama wote wa kufuga pamoja
na nyara kutoka kwenye miji yao tulichukua
vikawa vyetu.

8 Hivyo kwa wakati huo tukachukua kutoka
kwa wafalme hawa wawili wa Waamori nchi ya
mashariki ya Yordani, kutoka Bonde la Arnoni
mpaka kufika kwenye Mlima Hermoni.
9 (Wasidoni huuita mlima huo Sirioni, nao
Waamori huuita Seniri.)
10 Tuliteka miji yote kwenye uwanda wa juu,
Gileadi yote, Bashani yote mpaka kufika Saleka
na Edrei, miji ya utawala wa Ogu huko Bashani.
11 (Mfalme Ogu wa Bashani ndiye peke yake
aliyesalia miongoni mwa mabaki ya Warefai.
Kitanda chake kilikuwa cha chuma chenye urefu
wa dhiraa tisa* na upana wa dhiraa nne.†
Mpaka sasa kinaweza kuonekana katika mji wa
Waamoni wa Raba.)

* **3:11** Dhiraa tisa ni sawa na mita 4. † **3:11** Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.

### *Mgawanyo Wa Nchi Mashariki Ya Yordani (Hesabu 32:1-42)*

12 Katika nchi tuliyoiteka wakati ule, niliwapa
kabila la Reubeni na Gadi eneo lililoko kaskazini
la Aroeri kando ya Bonde la Arnoni, na nusu ya
eneo la milima ya Gileadi, pamoja na miji yake.
13 Kisha nusu ya kabila la Manase niliwapa
sehemu ya Gileadi iliyobaki pamoja na Bashani
yote, ambayo ilikuwa utawala wa Ogu. (Eneo
lote la Argobu katika Bashani lilikuwa linaju-
likana kama nchi ya Warefai.
14 Yairi, mzao wa kabila la Manase, alichukua
eneo lote la nchi ya Argobu hadi kufikia mpaka
wa Wageshuri na Wamaaka, ukaitwa kwa jina
lake; kwa hiyo mpaka leo hii Bashani inaitwa
Hawoth-Yairi.)
15 Nikampa Makiri nchi ya Gileadi.
16 Lakini niliwapa Wareubeni na Wagadi eneo
kuanzia Gileadi hadi Bonde la Arnoni (katikati
ya bonde ulikuwa ndio mpaka), kuelekea mpaka
Mto Yaboki, ambao ndio mpaka wa Waamoni.
17 Kwa upande wa magharibi mpaka wao
ulikuwa Yordani katika Araba, toka ziwa
Galilaya hadi Bahari ya Araba (yaani Bahari ya
Chumvi), kwenye miteremko ya Pisga upande wa
mashariki.
18 Wakati huo nilikuamuru: "BWANA Mungu
wako amekupa nchi hii uimiliki. Lakini ni laz-
ima wanaume wenu wote wenye uwezo, wakiwa
wamejiandaa tayari kwa vita, wavuke ng'ambo
wakiwatangulia ndugu zako Waisraeli.
19 Lakini wake zenu, watoto wenu na mifugo
yenu (kwani najua mnayo mifugo mingi)

wanaweza kukaa katika miji niliyowapa,
20 mpaka hapo BWANA atakapowapa ndugu zenu kupumzika kama alivyowapa ninyi, wao pia wamiliki ile nchi ambayo BWANA Mungu wenu anawapa, ng'ambo ya Yordani. Baada ya hapo, kila mmoja wenu anaweza kurudi kwenye milki niliyowapa."

### *Mose Akatazwa Kuvuka Yordani*

21 Wakati huo nilimwamuru Yoshua, "Umejionea kwa macho yako mwenyewe yale yote ambayo BWANA Mungu wenu amewafanyia wafalme hawa wawili. BWANA atazifanyia falme zote huko mnakokwenda vivyo hivyo.
22 Msiwaogope, BWANA Mungu wenu atapigana kwa ajili yenu."
23 Wakati huo nilimsihi BWANA:
24 "Ee BWANA Mwenyezi, umemwonyesha mtumishi wako ukuu wako na mkono wako wenye uweza. Kwa kuwa ni mungu yupi aliye mbinguni au duniani anayeweza kufanya kazi na matendo makuu kama ufanyayo wewe?
25 Acha niende nikaione hiyo nchi nzuri ng'ambo ya Yordani, ile nchi nzuri ya vilima na Lebanoni."
26 Lakini kwa sababu yenu BWANA alinikasirikia na hakutaka kunisikiliza. BWANA aliniambia, "Hilo latosha; usiseme nami jambo hili tena.
27 Kwea juu ya kilele cha Pisga uangalie magharibi, kaskazini, kusini na mashariki. Iangalie hiyo nchi kwa macho yako, kwa vile wewe hutavuka Yordani.

28 Lakini mwagize Yoshua, mtie moyo na umtie
nguvu, kwa kuwa yeye atawaongoza watu hawa
hadi ng'ambo na kuwarithisha nchi utakay-
oiona."
29 Kwa hiyo tulikaa kwenye bonde karibu na
Beth-Peori.

# 4

*Waamriwa Utii*

1 Sikia sasa, ee Israeli, amri na sheria nitaka-
zokufundisha wewe. Zifuate ili upate kuishi na
uingie kuimiliki nchi ambayo BWANA, Mungu wa
baba zako anawapa.
2 Usiongeze wala usipunguze chochote nina-
chowaamuru ninyi, ila myashike maagizo ya
BWANA Mungu wenu ambayo nawapa.
3 Mliona kwa macho yenu wenyewe kile
BWANA alichokifanya kule Baal-Peori. BWANA
Mungu wenu aliwaangamiza kutoka miongoni
mwenu kila mmoja aliyemfuata Baali wa Peori,
4 lakini ninyi nyote mlioshikamana na BWANA
kwa uthabiti, Mungu wenu, mko hai mpaka leo.
5 Tazama, nimewafundisha amri na sheria
kama BWANA Mungu wangu alivyoniamuru
mimi, ili mzifuate katika nchi mnayoiingia kuim-
iliki.
6 Zishikeni kwa uangalifu, kwa kuwa hii
itaonyesha hekima na ufahamu wenu kwa
mataifa, ambayo yatasikia kuhusu amri zote hizi,
nao watasema, "Hakika taifa hili kubwa ni watu
wenye hekima na ufahamu."
7 Ni taifa gani jingine lililo kubwa kiasi cha
kuwa na miungu yao iliyo karibu nao kama

BWANA Mungu wetu alivyo karibu nasi wakati
wowote tunapomwomba?
8 Nalo ni taifa gani jingine lililo kubwa hivi
lenye kuwa na amri na sheria za haki kama hizi
ninazoweka mbele yenu leo?
9 Mwe waangalifu, na makini ili msije mkasa-
hau mambo ambayo mliyaona kwa macho yenu,
wala kuyaacha yaondoke moyoni mwenu siku
zote za uhai wenu. Mwafundishe hayo watoto
wenu na watoto wao baada yao.
10 Kumbuka siku uliyosimama mbele za BWANA
Mungu wako kule Horebu, wakati aliponiambia,
“Wakutanishe watu mbele yangu wasikie ma-
neno yangu ili kwamba waweze kujifunza ku-
niheshimu kwa muda wote watakaoishi katika
nchi, nao waweze kuwafundisha watoto wao
maneno hayo.”
11 Mlisogea karibu na mkasimama chini ya
mlima wakati ulipowaka moto mpaka mbinguni
juu, pamoja na mawingu meusi na giza nene.
12 Ndipo BWANA alipozungumza nanyi ku-
toka moto. Mkasikia sauti ya maneno lakini
hamkuona umbo, kulikuwa na sauti tu.
13 Aliwatangazia Agano lake na Amri
Kumi, ambazo aliwaamuru mzifuate, kisha
akaziandika juu ya vibao viwili vya mawe.
14 Naye BWANA alinielekeza wakati huo kuwa-
fundisha ninyi sheria na amri ambazo mna-
paswa kuzifuata katika nchi ambayo mnavuka
Yordani kuimiliki.

### *Kuabudu Sanamu Kwakatazwa*

15 Hamkuona umbo la aina yoyote siku am-
bayo BWANA alizungumza nanyi kule Horebu

kutoka kwenye moto. Kwa hiyo mjihadhari kwa uangalifu sana,
16 ili msije mkajichafua na kujitengenezea sanamu au kinyago chenye umbo lolote kama la mwanaume au mwanamke,
17 au kama mnyama aliye juu ya nchi au ndege yeyote arukaye angani,
18 au kama kiumbe kitambaacho juu ya ardhi au samaki yeyote aliye ndani ya maji.
19 Na utazamapo juu angani na ukaliona jua, mwezi na nyota na vyote vinavyoipamba mbingu, usije ukashawishiwa kuviinamia na kuviabudu vile ambavyo BWANA Mungu wenu alivyogawia mataifa yote chini ya mbingu.
20 Lakini kwenu ninyi, BWANA amewatoa kutoka kwenye tanuru ya kuyeyushia chuma, katika Misri kuwa watu wa urithi wake kama mlivyo sasa.
21 BWANA alinikasirikia kwa sababu yenu na akaapa kwamba sitavuka Yordani kuingia katika nchi nzuri BWANA Mungu wenu anayowapa kuwa urithi wenu.
22 Nitakufa katika nchi hii; sitavuka Yordani, lakini ninyi ni karibu mvuke mkaimiliki ile nchi nzuri.
23 Jihadharini msilisahau Agano la BWANA Mungu wenu lile alilofanya nanyi; msijitengenezee sanamu katika umbo la kitu chochote ambacho BWANA Mungu wenu amewakataza.
24 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu ni moto ulao, Mungu mwenye wivu.
25 Baada ya kuwa na watoto na wajukuu na kuishi katika nchi hiyo siku nyingi, tena kama

mkijichafua na kutengeneza sanamu ya aina
yoyote, mkifanya maovu machoni pa BWANA
Mungu wenu na kumfanya awe na hasira,
26 ninaziita mbingu na nchi kama mashahidi
dhidi yenu siku hii kwamba mtaangamia mara
moja kutoka nchi ile ambayo mnavuka Yordani
kuimiliki. Hamtaishi kule kwa muda mrefu bali
kwa hakika mtaangamizwa.
27 BWANA atawatawanya miongoni mwa
mataifa, na ni wachache wenu tu watakaosalia
miongoni mwa mataifa hayo ambayo BWANA
atawafukuzia.
28 Huko mtaabudu miungu ya miti na mawe
iliyotengenezwa na watu, ambayo haiwezi
kuona au kusikia wala kula au kunusa.
29 Lakini kama mtamtafuta BWANA Mungu
wenu, mtampata; kama mtamtafuta kwa moyo
wenu wote na kwa roho yote.
30 Wakati mnapokuwa katika dhiki, nayo
mambo haya yote yamewatokea siku hizo, ndipo
mtamrudia BWANA Mungu wenu na kumtii.
31 Kwa maana BWANA Mungu wenu ni
Mungu mwenye huruma, hatawaacha au
kuwaangamiza wala kusahau Agano alilofanya
na baba zenu, alilowathibitishia kwa kiapo.

### *BWANA Ndiye Mungu*

32 Sasa uliza kuhusu siku za zamani, zamani
kabla ya wakati wako, tangu siku ile Mungu
alipomuumba mtu juu ya nchi, uliza kutoka
mwisho mmoja wa mbingu mpaka mwisho
mwingine wa mbingu. Je, kumepata kutokea
jambo jingine lililo kubwa kama hili, au kuna
jambo jingine kama hilo limepata kusikiwa?

33 Je, kuna watu wengine wowote waliosikia
sauti ya Mungu ikizungumza kwenye moto,
kama mlivyosikia, nao wakaishi?
34 Je, kuna mungu yeyote amepata kujaribu
mwenyewe kuchukua taifa moja kutoka taifa
lingine, kwa mapigo, kwa ishara za miujiza na
maajabu, kwa vita, kwa mkono wenye nguvu na
mkono ulionyooshwa au kwa matendo makuu ya
kutisha, kama yale ambayo BWANA Mungu wenu
aliyofanya kwa ajili yenu huko Misri mbele ya
macho yenu?

35 Mlionyeshwa mambo haya ili mpate kujua
kuwa BWANA ndiye Mungu; hakuna mwingine
ila yeye.
36 Kutoka mbinguni amewasikizisha sauti yake
ili kuwaadilisha. Hapa duniani aliwaonyesha
moto wake mkubwa, nanyi mlisikia maneno
yake kutoka kwenye ule moto.
37 Kwa sababu aliwapenda baba zenu na alich-
agua wazao wao baada yao, aliwatoa katika nchi
ya Misri kwa Uwepo wake na kwa uwezo wake
mkuu,
38 aliwafukuza mbele yenu mataifa makubwa
na yenye nguvu kuliko ninyi na kuwaleta ninyi
katika nchi yao na akawapa ninyi kuwa urithi
wenu, kama ilivyo leo.

39 Kubalini na mweke moyoni leo kuwa BWANA
ndiye Mungu mbinguni juu na duniani chini.
Hakuna mwingine.
40 Mshike amri na maagizo yake ninayowapa
leo, ili mpate kufanikiwa ninyi na watoto wenu
baada yenu, na mpate kuishi maisha marefu

katika nchi awapayo BWANA Mungu wenu siku zote.

### *Miji Ya Makimbilio*

41 Kisha Mose akatenga miji mitatu mashariki ya Yordani,
42 ambayo mtu yeyote aliyemuua mtu angeweza kukimbilia ikiwa amemuua jirani yake bila kukusudia na bila kuwa na chuki naye siku zilizopita. Angeweza kukimbilia katika mmojawapo ya miji hii na kuokoa maisha yake.
43 Miji hiyo ilikuwa: Bezeri katika tambarare ya jangwa kwa ajili ya Wareubeni; Ramothi katika nchi ya Gileadi kwa ajili ya Wagadi; nao mji wa Golani katika nchi ya Bashani kwa ajili ya Wamanase.

### *Utangulizi Wa Sheria*

44 Hii ndiyo sheria Mose aliyoweka mbele ya Waisraeli.
45 Haya ndiyo masharti, amri na sheria Mose aliyowapa wana wa Israeli wakati walitoka Misri,
46 nao walikuwa katika bonde karibu na Beth-Peori mashariki ya Yordani, katika nchi ya Sihoni mfalme wa Waamori, ambaye alitawala Heshboni, naye alishindwa na Mose na Waisraeli walipokuja toka Misri.
47 Waliimiliki nchi yake na nchi ya Ogu mfalme wa Bashani, wafalme wawili Waamori waliotawala mashariki ya Yordani.
48 Nchi hii ilienea kutoka Aroeri ukingoni mwa Bonde la Arnoni mpaka Mlima Sioni (yaani Hermoni),

49 pamoja na eneo lote la Araba mashariki
ya Yordani, na kuenea mpaka Bahari ya Araba
kwenye miteremko ya Pisga.

# 5

### *Amri Kumi*
### *(Kutoka 20:1-17)*

1 Mose akawaita Israeli wote, akawaambia:
Ee Israeli, sikilizeni amri na sheria ninazowatangazia leo. Jifunzeni, na mwe na hakika kuzifuata.
2 BWANA Mungu wetu alifanya Agano nasi
katika mlima wa Horebu.
3 Si kwamba BWANA alifanya Agano na baba
zetu, bali alifanya nasi, nasi sote ambao tuko hai
hapa leo.
4 BWANA alisema nanyi uso kwa uso kutoka
moto juu ya mlima.
5 (Wakati huo nilisimama kati ya BWANA na
ninyi kuwatangazia neno la BWANA, kwa sababu
mliogopa ule moto, nanyi hamkupanda mlimani.) Naye Mungu alisema:

6 "Mimi ndimi BWANA Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka nchi ya utumwa.
7 Usiwe na miungu mingine ila mimi.
8 Usijitengenezee sanamu katika umbo la kitu chochote kilicho juu mbinguni au duniani chini au ndani ya maji.
9 Usivisujudie wala kuviabudu; kwa kuwa
Mimi, BWANA Mungu wako, ni Mungu mwenye
wivu, ninayewaadhibu watoto kwa ajili ya

dhambi za baba zao hadi kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,
10 lakini ninaonyesha upendo kwa maelfu ya vizazi vya wale wanipendao na kuzishika amri zangu.
11 Usilitaje bure jina la BWANA Mungu wako, kwa kuwa BWANA hataacha kumhesabia hatia yeye alitajaye jina lake bure.
12 Adhimisha siku ya Sabato na kuiweka takatifu, kama BWANA Mungu wako alivyokuagiza.
13 Kwa siku sita utafanya kazi na kutenda shughuli zako zote.
14 Lakini siku ya Saba ni Sabato kwa BWANA, Mungu wako. Siku hiyo hutafanya kazi yoyote, wewe, wala mwanao au binti yako, wala mtumishi wa kiume au mtumishi wa kike, wala ng'ombe wako, punda wako au mnyama wako yeyote, wala mgeni aliyeko malangoni mwako, ili kwamba mtumishi wako wa kiume na wa kike wapate kupumzika kama wewe.
15 Kumbuka mlikuwa watumwa huko Misri, na BWANA Mungu wenu aliwatoa huko kwa mkono wenye nguvu na kwa mkono ulionyooshwa. Kwa hiyo BWANA Mungu wako amekuagiza kuiadhimisha siku ya Sabato.
16 Waheshimu baba yako na mama yako, kama BWANA Mungu wako alivyokuagiza, ili siku zako zipate kuwa nyingi na kufanikiwa katika nchi BWANA Mungu wako anayokupa.
17 Usiue.
18 Usizini.
19 Usiibe.
20 Usimshuhudie jirani yako uongo.

21 Usitamani mke wa jirani yako. Usitamani
nyumba ya jirani yako au shamba lake, mtu-
mishi wake wa kiume au wa kike, ng'ombe
au punda wake, wala kitu chochote cha
jirani yako."

22 Hizi ndizo amri alizozitangaza BWANA kwa
sauti kubwa kwa kusanyiko lenu lote huko
mlimani kutoka kwenye moto, wingu na giza
nene, wala hakuongeza chochote zaidi. Kisha
akaziandika juu ya vibao viwili vya mawe, naye
akanipa mimi.

### *Woga Wa Watu Mlimani (Kutoka 20:18-21)*

23 Mliposikia sauti kutoka kwenye giza, mlima
ulipokuwa ukiwaka moto, viongozi wenu wote
wa makabila yenu na wazee wenu walinijia
mimi.
24 Nanyi mkasema, "BWANA Mungu wetu ame-
tuonyesha utukufu na enzi yake, nasi tumesikia
sauti yake kutoka kwenye moto. Leo tume-
ona kwamba mwanadamu anaweza kuishi hata
kama Mungu akizungumza naye.
25 Lakini sasa, kwa nini tufe? Moto huu
mkubwa utatuteketeza sisi na tutakufa kama
tukiendelea kusikia sauti ya BWANA Mungu wetu
zaidi.
26 Ni mtu yupi mwenye mwili ambaye ame-
wahi kuisikia sauti ya Mungu aliye hai ak-
izungumza kutoka kwenye moto, kama sisi
tulivyoisikia, naye akaishi?
27 Sogea karibu usikie yale yote asemayo
BWANA Mungu wetu. Kisha utuambie chochote

kile ambacho BWANA Mungu wetu anakuambia.
Tutasikiliza na kutii.”
28 BWANA aliwasikia wakati mlipozungumza
nami, na BWANA akaniambia, “Nimesikia kile
hawa watu walichokuambia. Kila kitu wali-
chokisema ni kizuri.
29 Laiti kama mioyo yao ingekuwa na
mwelekeo wa kuniogopa na kuzishika amri
zangu zote daima, ili kwamba wafanikiwe wao
pamoja na watoto wao milele!
30 “Nenda uwaambie warudi kwenye mahema
yao.
31 Lakini wewe baki hapa pamoja nami ili
niweze kukupa maagizo yote, amri na sheria
ambazo utawafundisha wazifuate katika nchi
ninayokwenda kuwapa waimiliki.”
32 Hivyo kuweni waangalifu kuyafanya yale
BWANA Mungu wenu aliyowaagiza; msigeuke
upande wa kuume wala wa kushoto.
33 Fuateni yale yote ambayo BWANA Mungu
wenu aliwaagiza, ili mpate kuishi, kustawi na
kuziongeza siku zenu katika nchi mtakayoimi-
liki.

# 6

### *Mpende BWANA Mungu Wako*

1 Haya ndiyo maagizo, amri na sheria ambazo
BWANA Mungu wenu aliniagiza niwafundishe
ninyi ili mpate kuyashika katika nchi ambayo
ninyi mnavuka Yordani kuimiliki,
2 ili kwamba ninyi, watoto wenu na watoto
wao baada yao wamche BWANA Mungu wenu
siku zote kwa kushika amri na maagizo yake

yote ninayowapa, ili mweze kuyafurahia maisha marefu.
3 Sikia, ee Israeli, nawe uwe mwangalifu kutii ili upate kufanikiwa na kuongezeka sana katika nchi itiririkayo maziwa na asali, kama BWANA, Mungu wa baba zenu, alivyowaahidi ninyi.
4 Sikia, ee Israeli: BWANA Mungu wako, BWANA ni mmoja.
5 Mpende BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.
6 Amri hizi ninazokupa leo zitakuwa katika moyo wako.
7 Wafundishe watoto wako kwa bidii. Nena kuhusu amri hizi uketipo nyumbani na wakati utembeapo njiani, ulalapo na uamkapo.
8 Zifunge kama alama juu ya mkono wako, na uzifunge juu ya paji la uso wako.
9 Ziandike kwenye miimo ya milango ya nyumba yako na juu ya malango yako.
10 Wakati BWANA Mungu wako atakapokuleta katika nchi aliyowaapia baba zako, Abrahamu, Isaki na Yakobo, kukupa wewe, nchi kubwa, ina miji inayopendeza ambayo hukuijenga,
11 nyumba zilizojaa vitu vizuri vya aina nyingi ambavyo hukuvijaza, visima ambavyo hukuchimba, na mashamba ya mizabibu na mizeituni ambayo hukupanda wewe, basi, utakapokula na kushiba,
12 jihadhari usije ukamwacha BWANA, aliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka nchi ya utumwa.
13 Utamcha BWANA Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake na kuapa kwa jina lake.

14 Usifuate miungu mingine, miungu ya mataifa yanayokuzunguka;
15 kwa kuwa BWANA Mungu wako, ambaye yuko katikati yako, ni Mungu mwenye wivu na hasira yake itawaka dhidi yako, naye atakuangamiza kutoka uso wa nchi.
16 Usimjaribu BWANA Mungu wako kama ulivyofanya huko Masa.
17 Utayashika maagizo ya BWANA Mungu wako kwa bidii, na masharti na amri alizokupa.
18 Fanya lililo haki na jema mbele za BWANA, ili upate kufanikiwa, uweze kuingia na kuimiliki nchi nzuri ambayo BWANA aliahidi kwa kiapo kwa baba zako,
19 kuwafukuza kwa nguvu adui zako mbele yako kama BWANA alivyosema.

20 Siku zijazo, mtoto wako atakapokuuliza, "Ni nini maana ya masharti haya, amri na sheria hizi ambazo BWANA Mungu wako alikuagiza wewe?"
21 Mwambie: "Tulikuwa watumwa wa Farao huko Misri, lakini BWANA alitutoa sisi kutoka Misri kwa mkono wenye nguvu.
22 BWANA akapeleka mbele yetu ishara za miujiza na maajabu makubwa na ya kutisha mno juu ya Misri na Farao pamoja na nyumba yake yote.
23 Lakini Mungu akatutoa huko, akatuleta na kutupa nchi hii ambayo aliwaahidi baba zetu kwa kiapo.
24 BWANA akatuagiza tutii amri hizi zote na kumcha BWANA Mungu wetu, ili tupate kustawi na kuendelea kuwa hai kama ilivyo leo.

25 Kama tukizitii kwa bidii amri hizi zote mbele
za Bwana Mungu wetu, kama alivyotuamuru
sisi, hiyo itakuwa haki yetu."

# 7

## *Kuyafukuza Mataifa*
## *(Kutoka 34:11-16)*

1 Bwana Mungu wako akuletapo katika nchi
unayoingia kuimiliki, na awafukuzapo mbele
yako mataifa mengi, yaani Wahiti, Wagirgashi,
Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi na
Wayebusi, mataifa saba makubwa tena yenye
nguvu kuliko wewe,
2 pia Bwana Mungu wako atakapowatia
mkononi mwako na ukawashinda, basi ni lazima
uwaangamize wote kabisa. Usifanye agano nao,
wala usiwahurumie.
3 Usioane nao. Usimtoe binti yako kuolewa na
mwanawe, au kumchukua binti yake aolewe na
mwanao.
4 Kwa maana watamgeuza mwanao aache
kunifuata, ili aitumikia miungu mingine, nayo
hasira ya Bwana itawaka dhidi yako, naye
atakuangamiza ghafula.
5 Hili ndilo utakalowafanyia: Vunja mad-
habahu yao, vunja mawe yao ya kuabudia,
katakata nguzo zao za Ashera na kuchoma
sanamu zao kwa moto.
6 Kwa kuwa wewe ni taifa takatifu kwa Bwana
Mungu wako. Bwana Mungu wako amekuch-
agua wewe kutoka mataifa yote juu ya uso wa
dunia kuwa watu wake, hazina yake ya thamani.

7 BWANA hakuweka upendo wake juu yenu na kuwachagua kwa sababu mlikuwa wengi mno kuliko watu wengine, kwa maana ninyi ndio mliokuwa wachache sana kuliko mataifa yote.
8 Lakini ni kwa sababu BWANA aliwapenda ninyi na kutunza kiapo alichowaapia babu zenu kwamba atawatoa ninyi kwa mkono wenye nguvu na kuwakomboa kutoka nchi ya utumwa, kutoka nguvu za Farao mfalme wa Misri.
9 Basi ujue kwamba BWANA Mungu wako ndiye Mungu; ni Mungu mwaminifu, anayetunza Agano la upendo kwa maelfu ya vizazi vya wale wanaompenda na kuzishika amri zake.
10 Lakini
kwa wale wanaomchukia
atawalipiza kwenye nyuso zao
kwa maangamizi;
hatachelewa kuwalipiza kwenye nyuso zao
wale wamchukiao.
11 Kwa hiyo, kuweni waangalifu kufuata maagizo, amri na sheria ninazowapa leo.

*Baraka Za Utiifu*
*(Kumbukumbu 28:1-14)*

12 Kama mkizingatia sheria hizi na kuzifuata kwa uangalifu, basi BWANA Mungu wenu atatunza Agano lake la upendo nanyi, kama alivyowaapia baba zenu.
13 Atawapenda ninyi na kuwabariki na kuongeza idadi yenu. Atabariki uzao wa tumbo lenu, mazao ya nchi yenu, nafaka, divai mpya na mafuta, ndama za ng'ombe wa makundi yenu, na kondoo za makundi yenu katika nchi ile aliyoapa kuwapa baba zenu.

14 Mtabarikiwa kuliko mataifa mengine
yote, hakuna wanaume wala wanawake
kwenu watakaokosa watoto, wala mifugo yenu
haitakuwa tasa.
15 BWANA atawakinga na kila ugonjwa. Mungu
hatatia juu yenu ugonjwa wowote mbaya mlio-
ufahamu huko Misri, lakini atatia ugonjwa juu
ya wale wote wanaokuchukia.
16 Ni lazima mwangamize watu wote am-
bao BWANA Mungu wenu atawatia mikononi
mwenu. Msiwatazame kwa kuwahurumia na
msiitumikie miungu yao, kwa kuwa itakuwa
mtego kwenu.

17 Mnaweza kujiuliza wenyewe “Mataifa haya
ni yenye nguvu kuliko sisi. Tutawezaje kuwa-
fukuza?”
18 Lakini msiwaogope. Kumbukeni vyema jinsi
BWANA Mungu wenu alivyofanya kwa Farao na
kwa wote huko Misri.
19 Mliona kwa macho yenu wenyewe majaribu
makubwa, ishara za miujiza na maajabu, mkono
wenye nguvu na ulionyooshwa, ambao kwa
huo BWANA Mungu wenu aliwatoa mtoke Misri.
BWANA Mungu wenu atawafanyia hivyo watu
wote ambao mnawaogopa sasa.
20 Zaidi ya hayo, BWANA Mungu wenu ata-
tuma manyigu miongoni mwao hadi yale mabaki
watakaojificha waangamie.
21 Msiingiwe na hofu kwa sababu yao, kwa
kuwa BWANA Mungu wenu, ambaye yupo mion-
goni mwenu ni mkuu naye ni Mungu wa kutisha.
22 BWANA Mungu wenu atawafukuza mataifa
hayo mbele yenu kidogo kidogo. Ham-

taruhusiwa kuwaondoa wote kwa mara moja, la sivyo wanyama mwitu wataongezeka na kuwa karibu nanyi.
23 Lakini BWANA Mungu wenu atawatia watu hao mikononi mwenu, akiwatia katika kuchanganyikiwa kukubwa mpaka wawe wameangamizwa.
24 Atawatia wafalme wao mikononi mwenu, nanyi mtayafuta majina yao chini ya mbingu. Hakuna hata mmoja atakayeweza kusimama dhidi yenu bali mtawaangamiza.
25 Vinyago vya miungu yao mtavichoma moto. Msitamani fedha wala dhahabu iliyo juu yao, wala msizichukue kwa ajili yenu, la sivyo mtakuwa mmetekwa navyo. Kwa kuwa ni chukizo kwa BWANA Mungu wenu.
26 Msilete vitu vya machukizo katika nyumba zenu kwani ninyi, mtatengwa kama vitu hivyo kwa maangamizo. Ukichukie kabisa kitu hicho kwa kuwa kimetengwa kwa maangamizo.

# 8

*Usimsahau BWANA*

1 Uwe mwangalifu kufuata kila agizo ninalokupa wewe leo, ili mweze kuishi, kuongezeka na mweze kuingia mkamiliki nchi ambayo BWANA aliahidi kwa kiapo kwa baba zenu.
2 Kumbuka jinsi BWANA Mungu wenu alivyowaongoza katika njia yote katika jangwa kwa miaka hii arobaini, kukunyenyekeza na kukujaribu ili ajue lililoko moyoni mwako, kwamba utayashika maagizo yake au la.

3 Alikudhili na kukufanya uone njaa kisha
akulishe kwa mana, ambayo wewe wala
baba zako hamkuijua, awafundishe kuwa
mwanadamu hataishi kwa mkate tu bali kwa
kila neno litokalo katika kinywa cha BWANA.
4 Nguo zenu hazikuchakaa wala miguu yenu
haikuvimba kwa miaka hii arobaini.
5 Mjue basi ndani ya mioyo yenu kama mtu
anavyomwadibisha mwanawe, ndivyo BWANA
Mungu wako atawaadibisha ninyi.

6 Shikeni maagizo ya BWANA Mungu wenu
mtembee katika njia zake na kumheshimu.
7 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu anawaleta
katika nchi nzuri, nchi yenye vijito na mabwawa
ya maji, yenye chemchemi zinazotiririka mabon-
deni na katika vilima;
8 nchi yenye ngano na shayiri, mizabibu na
mitini, mikomamanga, mafuta ya zeituni na
asali;
9 nchi ambayo chakula hakitapungua na ham-
takosa chochote; nchi ambayo miamba yake ni
chuma na mnaweza kuchimba shaba kutoka
kwenye vilima.

10 Wakati mtakapokwisha kula na kushiba,
msifuni BWANA Mungu wenu kwa ajili ya nchi
nzuri aliyowapa.
11 Jihadharini msimsahau BWANA Mungu
wenu, mkashindwa kushika maagizo yake, she-
ria na amri zake ambazo ninawapa leo.
12 Angalia wakati mtakapokuwa mmekula na
kushiba, mkajenga nyumba nzuri na kukaa
humo,

13 na wakati makundi yenu ya ng'ombe na mbuzi na kondoo yatakapoongezeka na fedha na dhahabu yenu itakapoongezeka na vyote mlivyo navyo vitakapozidishwa,

14 basi mioyo yenu isiwe na kiburi mkamsahau BWANA Mungu wenu aliyewatoa katika nchi ya Misri, kutoka nchi ya utumwa.

15 Aliwaongoza kupitia jangwa lile kubwa na la kutisha, nchi ile ya kiu isiyo na maji, yenye nyoka wa sumu na nge. Aliwatolea maji kutoka kwenye mwamba mgumu.

16 Aliwapa mana ya kula jangwani, kitu ambacho baba zenu hawakukijua, ili kuwanyenyekesha na kuwajaribu ninyi ili mwishoni apate kuwatendea mema.

17 Mnaweza kusema, "Uwezo wangu na nguvu za mikono yangu ndizo zilizonipatia utajiri huu."

18 Lakini kumbukeni BWANA Mungu wenu, ndiye ambaye huwapa uwezo wa kupata utajiri, na hivyo kulithibitisha Agano lake, ambalo aliwaapia baba zenu, kama ilivyo leo.

19 Ikiwa mtamsahau BWANA Mungu wenu, mkaifuata miungu mingine, mkaiabudu na kuisujudia, ninashuhudia dhidi yenu leo kwamba hakika mtaangamizwa.

20 Kama mataifa BWANA aliyoyaangamiza mbele yenu, ndivyo ninyi mtakavyoangamizwa kwa kutokumtii BWANA Mungu wenu.

# 9

### *Si Kwa Sababu Ya Haki Ya Waisraeli*
*(Kutoka 32:1-35)*

1 Sikiliza, ee Israeli. Sasa mnakaribia kuvuka Yordani mwingie na kuwafukuza mataifa makubwa na yenye nguvu kuliko ninyi pamoja na miji mikubwa yenye kuta zilizofika juu angani.
2 Watu ni wenye nguvu na warefu, ni wana wa Waanaki! Mnafahamu habari zao na mmesikia inavyosemekana: "Ni nani awezaye kusimama dhidi ya Waanaki?"
3 Kuweni na hakika leo kwamba BWANA Mungu wenu ndiye atakayetangulia kuvuka mbele yenu kama moto uteketezao. Atawaangamiza; atawatiisha mbele yenu. Nanyi mtawafukuza na kuwaangamiza mara moja, kama BWANA alivyowaahidi.
4 Baada ya BWANA Mungu wenu kuwafukuza mbele yenu, msiseme mioyoni mwenu, "BWANA ametuleta hapa kuimiliki nchi hii kwa sababu ya haki yetu." La, ni kwa sababu ya uovu wa mataifa haya ndiyo BWANA anawafukuza mbele yenu.
5 Si kwa sababu ya haki yenu wala uadilifu wenu kwamba mtaimiliki nchi yao; lakini kwa sababu ya uovu wa mataifa haya, BWANA Mungu wenu atawafukuza mbele yenu, ili kutimiza lile alilowaapia baba zenu Abrahamu, Isaki na Yakobo.
6 Basi mjue, si kwa sababu ya haki yenu BWANA Mungu wenu anawapa nchi hii nzuri kuimiliki, kwa kuwa ninyi ni taifa lenye shingo ngumu.

### *Ndama Ya Dhahabu*

7 Kumbukeni hili, kamwe msisahau jinsi mlivyomkasirisha BWANA Mungu wenu kwa hasira

huko jangwani. Tangu siku mlipotoka Misri mpaka mlipofika hapa, mmekuwa waasi dhidi ya BWANA.

8 Kule Horebu mliamsha ghadhabu ya BWANA, kwa hiyo alikasirika vya kutosha hata akataka kuwaangamiza.

9 Nilipopanda mlimani kupokea mbao za mawe, mbao za Agano lile BWANA alilofanya nanyi, nilikaa mlimani siku arobaini usiku na mchana, sikula mkate wala sikunywa maji.

10 BWANA alinipa mbao mbili za mawe zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu. Juu ya mbao hizo kulikuwepo amri zote ambazo BWANA aliwatangazia kule mlimani kwa njia ya moto, siku ya kusanyiko.

11 Mwisho wa siku arobaini usiku na mchana, BWANA alinipa mbao mbili za mawe, mbao za Agano.

12 Kisha BWANA akaniambia, “Shuka chini mara moja, kwa sababu watu wako ambao umewatoa katika nchi ya Misri wamepotoka. Wamegeukia mbali haraka kutoka lile nililowaagiza, wamejitengenezea sanamu ya kusubu.”

13 Naye BWANA akaniambia, “Nimewaona watu hawa nao ni watu wenye shingo ngumu sana!

14 Niache, ili nipate kuwaangamiza na kufuta jina lao kutoka chini ya mbingu. Nami nitakufanya kuwa taifa lenye nguvu zaidi na kuwa wengi kuliko wao.”

15 Kwa hiyo niligeuka na kuteremka kutoka mlimani kwani mlima ulikuwa ukiwaka moto. Pia vibao vile viwili vya Agano vilikuwa mikononi mwangu.

16 Nilipotazama, niliona kuwa mmefanya dhambi dhidi ya BWANA Mungu wenu; mmejifanyia sanamu ya kusubu katika umbo la ndama. Mmegeuka upesi kutoka njia ile BWANA aliyowaagiza.
17 Kwa hiyo nilichukua vibao vile viwili nikavitupa na kuvipasua vipande vipande mbele ya macho yenu.

18 Ndipo tena nikasujudu mbele za BWANA kwa siku arobaini usiku na mchana. Sikula mkate wala sikunywa maji, kwa sababu ya dhambi yote mliyoifanya, mkifanya lile lililo ovu mbele za BWANA na kumkasirisha.
19 Niliogopa hasira na ghadhabu ya BWANA, kwa kuwa aliwakasirikia vya kutosha na kutaka kuwaangamiza. Lakini BWANA alinisikiliza tena.
20 Bali yeye alimkasirikia Aroni kiasi cha kutaka kumwangamiza, nami wakati huo nilimwombea Aroni pia.
21 Kisha nikachukua ile sanamu ya ndama mliyoitengeneza na kuichoma kwenye moto. Nikaiponda na kuisaga ikawa unga laini kama vumbi, nikatupa lile vumbi kwenye kijito kilichotiririka toka mlimani.
22 Pia mlimkasirisha BWANA huko Tabera, Masa na Kibroth-Hataava.
23 Vilevile wakati BWANA alipowatuma kutoka Kadesh-Barnea, alisema, “Kweeni, mkaimiliki nchi ambayo nimewapa.” Lakini mliasi dhidi ya agizo la BWANA Mungu wenu. Hamkumtegemea wala kumtii.
24 Mmekuwa waasi dhidi ya BWANA tangu nilipowajua ninyi.

25 Nilianguka kifudifudi mbele za BWANA
kwa zile siku arobaini usiku na mchana
kwa sababu BWANA alikuwa amesema ange-
waangamiza ninyi.
26 Nilimwomba BWANA na kusema, “Ee BWANA
Mwenyezi, usiangamize watu wako, urithi wako
mwenyewe ule ulioukomboa kwa uweza wako
mkuu na kuwatoa katika nchi ya Misri kwa
mkono wenye nguvu.
27 Wakumbuke watumishi wako Abrahamu,
Isaki na Yakobo. Usiangalie ukaidi wa watu
hawa, uovu wao wala dhambi yao.
28 Watu wa nchi ile uliyotutoa sisi
wasije wakasema, ‘Ni kwa sababu BWANA
hakuweza kuwachukua mpaka nchi aliyokuwa
amewaahidia, kwa sababu aliwachukia,
akawaleta ili aje kuwaua jangwani.’
29 Bali wao ni watu wako, urithi wako ule
ulioutoa Misri kwa uweza wako mkuu na kwa
mkono wako ulionyooka.”

# 10

### *Vibao Vingine Vya Amri Kumi (Kutoka 34:1-10)*

1 Wakati ule BWANA aliniambia, “Chonga vibao
viwili vya mawe kama vile vya kwanza uje
kwangu juu mlimani. Pia utengeneze Sanduku
la mbao.
2 Nitaandika juu ya vibao maneno yaliyokuwa
katika vile vibao vya kwanza, ambavyo uli-
vivunja. Kisha utaviweka ndani ya Sanduku.”
3 Hivyo nikatengeneza Sanduku kwa mti
wa mshita, nikachonga pia vibao vya mawe

kama vile vya kwanza, kisha nikakwea mlimani
nikiwa na vibao viwili mikononi mwangu.
4 BWANA akaandika juu ya hivi vibao kile
alichokuwa amekiandika kabla, Amri Kumi al-
izokuwa amewatangazia juu mlimani, kutoka
kwenye moto siku ile ya kusanyiko. BWANA
akanikabidhi.
5 Kisha nikashuka kutoka mlimani na kuweka
vibao ndani ya Sanduku nililokuwa nimeliten-
geneza, kama BWANA alivyoniagiza, navyo viko
huko sasa.
6 (Waisraeli walisafiri kutoka visima vya
Yaakani hadi Mosera. Huko Aroni alifariki na
kuzikwa, naye Eleazari mwanawe akachukua
nafasi yake kama kuhani.
7 Kutoka pale, walisafiri hadi Gudgoda
wakaendelea mpaka Yotbatha, nchi yenye vijito
vya maji.
8 Wakati huo BWANA aliteua kabila la Lawi
kulibeba Sanduku la Agano la BWANA, kusimama
mbele za BWANA ili kutoa huduma, na kutangaza
baraka kwa Jina lake, kama wanavyofanya
mpaka leo.
9 Hiyo ndiyo sababu ya Walawi kutokuwa na
sehemu wala urithi miongoni mwa ndugu zao;
BWANA ndiye urithi wao, kama BWANA Mungu
wao alivyowaambia.)
10 Basi nilikaa mlimani kwa siku arobaini
usiku na mchana, kama nilivyofanya mara ya
kwanza, pia BWANA alinisikiliza hata wakati huu.
Haikuwa nia yake kuwaangamiza.
11 BWANA akaniambia, “Nenda, ukawaongoze
watu katika njia yao ili kwamba waweze kuingia

na kuimiliki nchi ile niliyowaapia baba zao kuwapa.”

### *Mche* BWANA

12 Na sasa, ee Israeli, BWANA Mungu wako anataka nini kwako ila kumcha BWANA Mungu wako, kwenda katika njia zake, kumpenda na kumtumikia BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote,
13 na kuyashika maagizo ya BWANA na amri zake ninazokupa leo kwa mafanikio yako mwenyewe?

14 Mbingu, hata mbingu za juu sana, dunia na kila kitu kilichomo ndani yake, ni mali ya BWANA Mungu wako.
15 Hata hivyo BWANA alikuwa na shauku na baba zako, akawapenda na akawachagua ninyi, wazao wao, kuliko mataifa yote, kama ilivyo leo.
16 Kwa hiyo tahirini mioyo yenu, na msiwe na shingo ngumu tena.
17 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu ni Mungu wa miungu na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye uweza na wa kutisha, ambaye hana upendeleo na hapokei rushwa.
18 Huwapigania yatima na wajane, humpenda mgeni, akimpa chakula na mavazi.
19 Nanyi wapendeni wageni, kwa kuwa ninyi wenyewe mlikuwa wageni huko Misri.
20 Mche BWANA Mungu wako na umtumikie yeye. Shikamana naye kwa uthabiti na kuapa kwa jina lake.

21 Yeye ni sifa yako; yeye ni Mungu wako, ambaye alikutendea yale maajabu makubwa na ya kutisha uliyoyaona kwa macho yako mwenyewe.
22 Baba zako walioshuka kwenda Misri jumla yao walikuwa sabini, na sasa BWANA Mungu wako amekufanya wengi kama nyota za angani.

# 11

### *Mpende Na Umtii BWANA*

1 Mpende BWANA Mungu wako na kushika masharti yake, amri zake, sheria zake na maagizo yake siku zote.
2 Kumbuka hivi leo kwamba sio watoto wako walioona na kujua adhabu ya BWANA Mungu wako: utukufu wake, mkono wake wenye nguvu, mkono wake ulionyooshwa;
3 ishara alizozifanya na mambo aliyoyafanya katikati ya Misri, kwa Farao mfalme wa Misri na kwa nchi yake yote;
4 lile alilolifanyia jeshi la Wamisri, farasi na magari yake, jinsi alivyowafurikisha na maji ya Bahari ya Shamu walipokuwa wakiwafuatilia ninyi, na jinsi BWANA alivyowaletea angamizo la kudumu juu yao.
5 Sio watoto wenu walioyaona yale Mungu aliyowafanyia huko jangwani mpaka mkafika mahali hapa,
6 wala lile Mungu alilowafanyia Dathani na Abiramu, wana wa Eliabu wa kabila la Reubeni, wakati ardhi ilipofungua kinywa chake katikati ya Israeli yote, ikawameza pamoja na walio

nyumbani mwao, hema zao na kila kitu kilichokuwa hai ambacho kilikuwa mali yao.

7 Bali ilikuwa ni macho yenu wenyewe ambayo yaliyaona mambo haya yote makuu BWANA aliyoyatenda.

8 Kwa hiyo fuateni maagizo yote ninayowapa leo, ili mpate kuwa na nguvu za kuingia na kuiteka nchi ile ambayo mnavuka Yordani kuimiliki,

9 ili mpate kuishi siku nyingi katika nchi ile ambayo BWANA aliapa kuwapa baba zenu na wazao wao, nchi itiririkayo maziwa na asali.

10 Nchi mnayoiingia kuimiliki haifanani na nchi ya Misri mlikotoka ambako mlipanda mbegu yenu na kuinywesha, kama bustani ya mboga.

11 Lakini nchi mnayovuka Yordani kuimiliki ni nchi ya milima na mabonde inywayo mvua kutoka mbinguni.

12 Ni nchi ambayo BWANA Mungu wenu anaitunza; macho ya BWANA Mungu wenu yanaitazama daima kutoka mwanzo wa mwaka hadi mwisho wa mwaka.

13 Hivyo kama mkiyatii maagizo yangu ninayowapa leo kwa uaminifu, yaani kwa kumpenda BWANA Mungu wenu, na kumtumikia kwa moyo wako wote na kwa roho yenu yote,

14 ndipo atawanyweshea mvua katika nchi yenu kwa majira yake, mvua ya masika na ya vuli, ili mpate kuvuna nafaka zenu, divai mpya na mafuta.

15 Nitawapa majani kwa ajili ya ng'ombe wenu, nanyi mtakula na kushiba.

16 Jihadharini, la sivyo mtashawishika
kugeuka na kuabudu miungu mingine na
kuisujudia.
17 Ndipo hasira ya BWANA itawaka dhidi yenu,
naye atafunga mbingu ili mvua isinyeshe nayo
ardhi haitatoa mazao, nanyi mtaangamia mara
katika nchi nzuri ambayo BWANA anawapa.
18 Yawekeni haya maneno yangu katika mioyo
yenu na akili zenu, yafungeni kama alama juu
ya mikono yenu na kwenye paji za nyuso zenu.
19 Wafundisheni watoto wenu, yazungumzeni
wakati mketipo nyumbani na wakati
mtembeapo njiani, wakati mlalapo na wakati
mwamkapo.
20 Yaandikeni juu ya miimo ya nyumba zenu
na juu ya malango yenu,
21 ili kwamba siku zenu na siku za watoto
wenu zipate kuwa nyingi katika nchi ile BWANA
aliyoapa kuwapa baba zenu, kama zilivyo nyingi
siku za mbingu juu ya nchi.
22 Kama mkishika kwa makini maagizo haya
yote ninayowapa kuyafuata, ya kumpenda
BWANA Mungu wenu, kuenenda katika njia zake
zote na kushikamana naye kwa uthabiti,
23 ndipo BWANA atawafukuza mataifa haya
yote mbele yako, nawe utawafukuza mataifa
yaliyo makubwa na yenye nguvu kukuliko
wewe.
24 Kila mahali mtakapoweka mguu wenu
patakuwa penu: Nchi yenu itaenea kutoka
jangwa la Lebanoni, na kutoka mto wa Frati hadi
bahari ya magharibi*

* **11:24** Yaani Bahari ya Mediterania.

25 Hapatakuwa na mtu atakayeweza kusi-
mama dhidi yenu. BWANA Mungu wenu, kama
alivyoahidi, ataweka juu ya nchi yote utisho na
hofu kwa ajili yenu popote mwendako.
26 Tazama, leo ninaweka mbele yenu baraka
na laana:
27 baraka kama mtatii maagizo ya BWANA
Mungu wenu, ambayo ninawapa leo;
28 laana kama hamtatii maagizo ya BWANA
Mungu wenu na kuacha njia ambayo ninawaa-
muru leo kwa kufuata miungu mingine, ambayo
hamkuijua.
29 Wakati BWANA Mungu wenu atakapokuwa
amewaleta katika nchi mnayoiingia kuimiliki,
mtatangaza baraka kutoka Mlima Gerizimu, na
kutangaza laana kutoka Mlima Ebali.
30 Kama mnavyofahamu, milima hii ipo
ng'ambo ya Yordani, magharibi ya barabara,
kuelekea machweo ya jua, karibu na miti
mikubwa ya More, katika nchi ya wale
Wakanaani wanaoishi Araba, jirani na Gilgali.
31 Karibu mvuke ng'ambo ya Yordani kuingia
na kuimiliki nchi ambayo BWANA Mungu wenu
anawapa. Wakati mtakapokuwa mmeichukua
na mnaishi humo,
32 hakikisheni kwamba mnatii amri na sheria
zote ninazoziweka mbele yenu leo.

# 12

### *Mahali Pekee Pa Kuabudia*

1 Hizi ndizo amri na sheria ambazo ni lazima
mwe waangalifu kuzifuata katika nchi ambayo

BWANA, Mungu wa baba zenu, amewapa kumiliki, kwa muda wote mtakaoishi katika nchi.

2 Haribuni kabisa kila mahali pao pa kuabudia kwenye milima mirefu, vilima na chini ya kila mti mkubwa ambamo mataifa haya mnayokwenda kuchukua ardhi yao huabudia miungu yao.

3 Bomoeni madhabahu zao, vunjeni yale mawe wanayoabudu, chomeni moto nguzo zao za Ashera; katilieni mbali sanamu za miungu yao na mfute majina yao mahali hapo.

4 Kamwe msimwabudu BWANA Mungu wenu kama wanavyoabudu wao.

5 Bali mtatafuta mahali BWANA Mungu wenu atakapopachagua katika makabila yenu yote ili aliweke jina lake huko kuwa makao yake. Mahali hapo ndipo iwapasapo kwenda;

6 hapo ndipo mtakapoleta sadaka zenu za kuteketezwa na dhabihu, zaka zenu na changizo zenu, kile ulichoweka nadhiri kutoa, sadaka zenu za hiari na malimbuko ya makundi yenu ya ng'ombe pamoja na mbuzi na kondoo.

7 Hapo, katika uwepo wa BWANA Mungu wenu, ninyi pamoja na jamaa zenu, mtakula na kufurahia kila kitu ambacho mmegusa kwa mikono yenu, kwa sababu BWANA Mungu wenu amewabariki.

8 Msifanye kama tunavyofanya hapa leo, kila mtu anavyopenda mwenyewe,

9 kwa kuwa bado hamjafikia mahali pa mapumziko na urithi ambao BWANA Mungu wenu anawapa.

10 Lakini mtavuka Yordani na kuishi katika nchi BWANA Mungu wenu anayowapa kama urithi, naye atawapa pumziko kutokana na adui zenu wote wanaowazunguka ili ninyi mpate kuishi kwa salama.
11 Kisha kuhusu mahali BWANA Mungu wenu atakapopachagua kuwa mahali pa makao ya Jina lake, hapo ndipo inapowapasa kuleta kila kitu ninachowaamuru: sadaka zenu za kuteketezwa na dhabihu, zaka zenu na changizo, pamoja na vitu vyote vyenye thamani ambavyo mmeweka nadhiri kumtolea BWANA.
12 Hapo furahini mbele za BWANA Mungu wenu, ninyi, wana wenu na binti zenu, watumishi wenu wa kiume na wa kike, pamoja na Walawi kutoka miji yenu ambao hawana mgawo wala urithi wao wenyewe.
13 Kuweni waangalifu, msitoe dhabihu zenu za kuteketezwa mahali popote mnapopapenda.
14 Mtazitoa tu mahali pale ambapo BWANA atachagua katika mojawapo ya makabila yenu, nanyi hapo zingatieni kila jambo ninalowaamuru.
15 Hata hivyo, mnaweza kuwachinja wanyama wenu katika miji yenu yoyote ile na kula nyama nyingi mpendavyo kama vile mmemchinja paa au kulungu, kulingana na baraka mtakazojaliwa na BWANA Mungu wenu. Watu walio najisi au walio safi wanaweza kula.
16 Lakini kamwe usinywe damu; imwage juu ya ardhi kama maji.
17 Hamruhusiwi kula katika miji yenu zaka yenu ya nafaka, ya divai mpya na ya mafuta, au mzaliwa wa kwanza wa makundi yenu ya

ng'ombe na makundi yenu ya mbuzi na kondoo, wala chochote ambacho mmeweka nadhiri kukitoa, au sadaka zako za hiari, wala matoleo maalum.
18 Badala yake, mtakula vitu hivyo katika uwepo wa BWANA Mungu wenu mahali ambapo BWANA Mungu wenu atapachagua: wewe, wana wako na binti zako, watumishi wako wa kiume na wa kike, na Walawi kutoka miji yenu. Mnatakiwa mfurahi mbele za BWANA Mungu wenu kwa kula kitu mtakachoweka mikono yenu.
19 Mwe waangalifu msiwapuuze Walawi kwa muda wote mnaoishi katika nchi yenu.

20 BWANA Mungu wenu atakapokuwa ameongeza nchi yenu kama alivyowaahidi, nanyi mkitamani nyama na mkisema, "Ningependa nyama," hapo unaweza kula nyingi upendavyo.
21 Kama mahali ambapo BWANA Mungu wenu atapachagua kuweka Jina lake ni mbali sana kutoka kwenu, unaweza kuchinja wanyama kutoka makundi yenu ya ng'ombe, ya mbuzi na ya kondoo ambayo BWANA amewapa, kama nilivyokuamuru, na mkiwa katika miji yenu wenyewe mnaweza kula nyingi mtakavyo.
22 Mle kama vile mngekula paa na kulungu. Wote walio najisi kiibada na walio safi mwaweza kula.
23 Lakini hakikisheni kwamba hamkunywa damu, kwa sababu damu ni uhai, kamwe msile uhai pamoja na nyama.
24 Hamruhusiwi kamwe kunywa damu; imwageni juu ya ardhi kama maji.

25 Msinywe damu, ili mweze kufanikiwa ninyi
pamoja na watoto wenu baada yenu, kwa
sababu mtakuwa mkifanya lililo haki machoni
pa BWANA.

26 Lakini vichukueni vitu vyenu vilivyowekwa
wakfu pamoja na vile mlivyoweka nadhiri,
mwende mahali pale BWANA atakapopachagua.
27 Leteni sadaka zenu za kuteketezwa juu
ya madhabahu ya BWANA Mungu wenu, vyote
nyama na damu. Damu ya dhabihu zenu laz-
ima imiminwe kando ya madhabahu ya BWANA
Mungu wenu, lakini nyama mnaweza kula.
28 Mwe waangalifu kutii masharti haya yote
ninayowapa, ili kwamba siku zote mweze ku-
fanikiwa, ninyi pamoja na watoto wenu baada
yenu, kwa sababu mtakuwa mkifanya lililo jema
na sahihi mbele za macho ya BWANA Mungu
wenu.

29 BWANA Mungu wenu atayakatilia
mbali mbele yenu mataifa ambayo punde
kidogo mtayavamia na kuyaondoa. Lakini
mtakapokuwa mmeyafukuza na kuishi katika
nchi yao,
30 na baada ya kuangamizwa mbele yenu, mwe
waangalifu msijiingize katika tanzi kwa kuuliza
habari za miungu yao, mkisema, "Je, mataifa
haya hutumikiaje miungu yao? Nasi tutafanya
vivyo hivyo."
31 Kamwe msimwabudu BWANA Mungu wenu
kwa njia wanayoabudu miungu yao, kwa sababu
katika kuabudu miungu yao, wanafanya aina
zote za machukizo anayoyachukia BWANA. Hata

huwateketeza wana wao na binti zao kwa moto
kama kafara kwa miungu yao.
32 Angalieni kwamba mnafanya yote niliy-
owaamuru; msiongeze kitu wala msipunguze
kitu.

# 13

*Kuabudu Miungu Mingine*

1 Kama nabii, au yule anayetabiri kwa njia
ya ndoto, akijitokeza miongoni mwenu na
akawatangazia ishara ya miujiza na ajabu,
2 ikiwa ishara au ajabu ya aliyozungumza
ikatokea, naye akasema, “Na tufuate miungu
mingine” (miungu ambayo hamjaifahamu) “na
tuiabudu,”
3 kamwe msiyasikilize maneno ya nabii wala
mwota ndoto huyo. BWANA Mungu wenu anawa-
jaribu kuangalia kama mnampenda kwa moyo
wenu wote na kwa roho yenu yote.
4 Ni BWANA Mungu wenu ambaye mnapaswa
kumfuata tena ni yeye mnapaswa kumheshimu.
Shikeni maagizo yake na kumtii, mtumikieni na
kushikamana naye.
5 Huyo nabii au mwota ndoto lazima auawe,
kwa sababu amehubiri uasi dhidi ya BWANA
Mungu wenu, ambaye aliwatoa kutoka nchi
ya Misri na kuwakomboa kutoka nchi ya
utumwa; amejaribu kuwageuza kutoka njia am-
bayo BWANA Mungu wenu aliwaagiza mfuate. Ni
lazima mwondoe uovu miongoni mwenu.
6 Kama ndugu yako hasa, au mwanao au binti
yako, au mke umpendaye, au rafiki yako wa
karibu sana akikushawishi kwa siri, akisema,

“Na twende tukaabudu miungu mingine” (mi-
ungu ambayo ninyi wala baba zenu hamkuifa-
hamu,
7 miungu ya watu wanaowazunguka, ikiwa
karibu au mbali, kutoka mwisho mmoja wa nchi
mpaka mwingine),
8 usikubali wala usimsikilize. Usimhurumie!
Usimwache wala usimkinge.
9 Hakika ni lazima auawe. Ni lazima mkono
wako uwe wa kwanza katika kumuua kisha
mikono ya watu wengine wote.
10 Mpigeni kwa mawe mpaka afe, kwa sababu
alijaribu kuwageuza mtoke kwa BWANA Mungu
wenu ambaye aliwatoa Misri, kutoka nchi ya
utumwa.
11 Kisha Israeli wote watasikia na kuo-
gopa, wala hakuna mmoja miongoni mwenu
atakayefanya uovu tena.
12 Kama mkisikia ikisemwa kwamba moja
ya miji ambayo BWANA Mungu wenu anawapa
mkae ndani yake
13 kuna wanaume waovu wameinuka mion-
goni mwenu na wamewapotosha watu wa
mji, wakisema, “Twendeni tukaabudu miungu
mingine” (miungu ambayo hamkuifahamu),
14 ndipo itakubidi kuuliza, kupima na kuchun-
guza kwa makini. Kama ni kweli, tena iki-
hakikishwa kwamba jambo hili lichukizalo lime-
fanyika miongoni mwenu,
15 kwa hakika ni lazima mwaue kwa upanga
wale wote wanaoishi katika mji ule. Uharibuni
kabisa, pamoja na watu wake na mifugo yake.
16 Kusanyeni nyara zote za mji katika uwanja
wa wazi na kuuchoma mji kabisa pamoja na

nyara zake zote kama sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA Mungu wenu. Utabaki kuwa magofu milele na hautajengwa tena.
17 Hakuna kimoja kati ya vitu vilivyolaaniwa kitakachokutwa mikononi mwenu, ili BWANA ageuze hasira yake kali. Atawahurumia na kuwa na rehema kwenu pia kuongeza idadi yenu, kama alivyowaahidi baba zenu,
18 kwa sababu mnamtii BWANA Mungu wenu, mkizishika amri zake zote zile ninazowapa leo na kufanya lile lililo jema machoni pake.

# 14

## *Vyakula Vilivyo Najisi Na Vilivyo Safi (Walawi 11:1-47)*

1 Ninyi ni watoto wa BWANA Mungu wenu. Msijichanje ama kujinyoa upara kwenye paji la uso kwa ajili ya aliyekufa,
2 kwa maana ninyi ni taifa takatifu kwa BWANA Mungu wenu. BWANA amewachagua ninyi kuwa taifa la kipekee kutoka mataifa yote juu ya uso wa dunia, mwe tunu yake.
3 Msile kitu chochote ambacho ni machukizo.
4 Hawa ndio wanyama mtakaokula: ng'ombe, kondoo, mbuzi,
5 kulungu, paa, kongoni, paa mweupe, mbuzi-mwitu, pofu na kondoo wa mlimani.
6 Mnaweza kumla mnyama yeyote mwenye kwato zilizogawanyika mara mbili, pia yule anayecheua.
7 Hata hivyo, miongoni mwa wale wanaocheua au wale walio na kwato zilizogawanyika kamwe msile ngamia, sungura na pelele.

Iwapo wanacheua, lakini hawana kwato
zilizogawanyika; ni najisi kwenu kwa taratibu
za kiibada.
8 Nguruwe pia ni najisi; ingawa ana kwato
zilizogawanyika, hacheui. Msile nyama yake
wala kugusa mzoga wake.

9 Katika viumbe hai vyote viishivyo kwenye
maji, mnaweza kula yeyote aliye na mapezi na
magamba.
10 Lakini chochote kisicho na mapezi na mag-
amba msile; kwenu ni najisi.

11 Mnaweza kula ndege yeyote aliye safi.
12 Lakini wafuatao msiwale: tai, furukombe,
kipungu,
13 kengewa mwekundu, kengewa mweusi,
mwewe wa aina yoyote,
14 kunguru wa aina yoyote,
15 mbuni, kiruka-njia, dudumizi, kipanga wa
aina yoyote,
16 bundi, mumbi, bundi mkubwa,
17 mwari, nderi, mnandi,
18 korongo, koikoi wa aina yoyote, hudihudi na
popo.
19 Wadudu wote warukao kwa makundi ni
najisi kwenu, msiwale.
20 Lakini viumbe vyote vyenye mabawa vilivyo
safi mwaweza kula.
21 Msile kitu chochote mtakachokuta kimekufa.
Mnaweza kumpa mgeni yeyote anayeishi katika
mojawapo ya miji yenu, naye anaweza kula
au mnaweza kumuuzia mtu wa nchi nyingine.
Lakini ninyi ni watu watakatifu kwa BWANA
Mungu wenu.

Msitokose mwana-mbuzi katika maziwa ya mama yake.

*Zaka*

22 Hakikisheni mmetenga sehemu ya kumi ya mazao yote ya mashamba yenu kila mwaka.
23 Mtakula zaka za nafaka yenu, divai mpya, mafuta na wazaliwa wa kwanza wa makundi yenu ya ng'ombe na ya kondoo na mbuzi mbele za BWANA Mungu wenu pale mahali atakapopachagua kama maskani kwa ajili ya Jina lake, ili kwamba mpate kujifunza kumheshimu BWANA Mungu wenu daima.
24 Lakini ikiwa mahali pale ni mbali sana nanyi mmebarikiwa na BWANA Mungu wenu na hamwezi kubeba zaka yenu (kwa sababu mahali pale BWANA atakapopachagua kuliweka Jina lake ni mbali sana),
25 basi badilisheni zaka yenu kuwa fedha, mkaichukue hiyo fedha mwende nayo mahali BWANA Mungu wenu atakapopachagua.
26 Tumieni hiyo fedha kununua chochote ukitakacho: ng'ombe, kondoo, divai au kinywaji chochote chenye chachu au chochote mnachotaka. Kisha ninyi na wa nyumbani mwenu mtaila mbele za BWANA Mungu wenu na kufurahi.
27 Msiache kuwajali Walawi waishio katika miji yenu, kwa kuwa hao hawana shamba wala urithi wao wenyewe.

28 Mwishoni mwa kila mwaka wa tatu, leteni zaka zote za mazao ya miaka ile na uyahifadhi kwenye miji yenu,

29 ili Walawi (ambao hawana mashamba wala
urithi wao wenyewe) na wageni, yatima na
wajane wanaoishi kwenye miji yenu wapate kuja
kula na kushiba, ili BWANA Mungu wenu apate
kuwabariki ninyi katika kazi zote za mikono
yenu.

# 15

## *Mwaka Wa Kufuta Madeni*
## *(Walawi 25:1-7)*

1 Kila mwisho wa miaka saba ni lazima mfute
madeni.
2 Hivi ndivyo itakavyofanyika: Kila mkope-
shaji atafuta mkopo aliomkopesha Mwisraeli
mwenzake. Hatamtaka Mwisraeli mwenzake au
ndugu yake amlipe hilo deni, kwa sababu wakati
wa BWANA wa kufuta madeni umetangazwa.
3 Unaweza kudai malipo kwa mgeni, lakini
lazima ufute kila deni ambalo unamdai ndugu
yako.
4 Hata hivyo, hapatakuwepo maskini miongoni
mwenu, kwa kuwa katika nchi BWANA Mungu
wenu anayowapa kuimiliki kama urithi wenu,
atawabariki sana,
5 ikiwa tutamtii BWANA Mungu wenu kikamil-
ifu na kuwa waangalifu kuyafuata maagizo haya
yote ninayowapa leo.
6 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu atawabariki
kama alivyoahidi, nanyi mtawakopesha
mataifa mengi lakini hamtakopa kwa yeyote.
Mtatawala mataifa mengi lakini hakuna taifa
litakalowatawala ninyi.

7 Ikiwa kuna mtu maskini miongoni mwa
ndugu zenu, katika mji wowote wa hiyo nchi am-
bayo Bwana Mungu wenu anawapa, msiwe na
moyo mgumu wala usimfumbie mkono ndugu
yako aliye maskini.
8 Afadhali fungua mikono yako na umkopeshe
kwa hiari chochote anachohitaji.
9 Jihadhari usijiwekee wazo hili ovu: "Mwaka
wa saba, mwaka wa kufuta madeni umekaribia,"
usije ukaonyesha nia mbaya kwa ndugu yako
mhitaji na ukaacha kumpa chochote. Anaweza
kumlalamikia Bwana dhidi yako nawe utakuwa
umepatikana na hatia ya dhambi.
10 Mpe kwa ukarimu na ufanye hivyo bila
kinyongo moyoni, ndipo kwa sababu ya hili
Bwana Mungu wenu atakubariki katika kazi
zako zote na kwa kila kitu utakachokiwekea
mkono wako.
11 Siku zote watakuwepo watu maskini katika
nchi. Kwa hiyo ninawaamuru mwe na
mikono iliyokunjuliwa kuwaelekea ndugu zenu,
kuwaelekea maskini na wahitaji katika nchi
yenu.

### *Kuwaacha Huru Watumwa (Kutoka 21:1-18)*

12 Kama Mwebrania mwenzako, mwanaume
au mwanamke, akijiuza kwako na kukutumikia
miaka sita, katika mwaka wa saba ni lazima
umwache aende zake akiwa huru.
13 Nawe wakati utakapomwachia usimwache
aende mikono mitupu.
14 Mpe kwa uhuru kutoka zizi lako la kondoo
na mbuzi, kutoka sakafu yako ya kupuria nafaka

na kutoka mashinikizo yako ya kukamulia divai. Mpe kama vile ambavyo BWANA Mungu wako alivyokubariki.
15 Kumbukeni kuwa ninyi mlikuwa watumwa huko Misri naye BWANA Mungu wenu aliwakomboa. Ndiyo sababu nimewapa agizo hili leo.
16 Lakini mtumishi wako akikuambia, "Sitaki kukuacha," kwa sababu anakupenda wewe na jamaa yako naye anaridhika nawe,
17 ndipo utachukua chuma kidogo utoboe sikio lake mpaka hicho chuma kiingie kwenye ubao wa mlango, naye atakuwa mtumishi wako wa maisha. Ufanye vivyo hivyo kwa mtumishi wa kike.
18 Usifikiri kuwa kuna ugumu kumwacha mtumishi wako huru, kwa sababu utumishi wake kwako kwa miaka hii sita umekuwa wa thamani mara mbili ya ujira wa mtumishi wa kuajiriwa. Naye BWANA Mungu wenu atakubarikia kwa kila kitu utakachofanya.

### *Wazaliwa Wa Kwanza Wa Wanyama*

19 Wekeni wakfu kwa BWANA Mungu wenu kila mzaliwa wa kwanza wa kiume wa makundi yenu ya ng'ombe na ya mbuzi na kondoo. Maksai walio wazaliwa wa kwanza msiwafanyize kazi, wala msinyoe manyoya ya wazaliwa wa kwanza wa kondoo.
20 Kila mwaka ninyi na jamaa zenu mtapaswa kuwala mbele za BWANA Mungu wenu pale mahali atakapopachagua.
21 Kama mnyama ana dosari, akiwa ni kilema au kipofu au kama ana kilema kibaya, kamwe usimtoe dhabihu kwa BWANA Mungu wenu.

22 Itawapasa kumla ninyi wenyewe katika miji
yenu. Wote wasio safi na walio safi kwa desturi
za kiibada mwaweza kula kama vile mnavyokula
paa au kulungu.
23 Lakini kamwe msinywe damu; imwageni
ardhini kama maji.

# 16

*Pasaka*
*(Kutoka 12:1-20)*

1 Shikeni mwezi wa Abibu, na kuiadhimisha
Pasaka ya BWANA Mungu wenu, kwa sababu
katika mwezi wa Abibu, Mungu aliwatoa Misri
usiku.
2 Mtatoa dhabihu ya Pasaka ya mnyama kwa
BWANA Mungu wenu kutoka kundi lenu la mbuzi
na kondoo au la ng'ombe, mahali pale ambapo
BWANA atapachagua kama makao kwa ajili ya
Jina lake.
3 Msile nyama hiyo pamoja na mikate iliyotiwa
chachu, lakini kwa siku saba mtakula mikate
isiyotiwa chachu, mikate ya kujitesa, kwa sababu
mliondoka Misri kwa haraka, ili kwamba siku
zote za maisha yenu mpate kukumbuka wakati
wenu wa kuondoka Misri.
4 Chachu isionekane katika mali zenu katika
nchi yenu yote kwa siku saba. Nyama yoyote
ya dhabihu mtakayotoa jioni ya siku ya kwanza
isibakizwe mpaka asubuhi.
5 Kamwe msitoe dhabihu ya Pasaka katika mji
wowote ambao BWANA Mungu wenu amewapa,
6 isipokuwa mahali atakapopachagua kama
makao kwa ajili ya Jina lake. Hapo ndipo lazima

mtoe dhabihu ya Pasaka jioni, jua litakapotua,
iwe kumbukumbu yenu ya kutoka Misri.
7 Okeni na mle mahali pale ambapo BWANA
Mungu wenu atakapopachagua, kisha asubuhi
mrudi kwenye mahema yenu.
8 Kwa siku sita mtakula mikate isiyotiwa
chachu na siku ya saba fanyeni kusanyiko kwa
ajili ya BWANA Mungu wenu na msifanye kazi.

### *Sikukuu Ya Mavuno (Kutoka 34:22; Walawi 23:15-21)*

9 Mhesabu majuma saba tangu wakati
mnapoanza kuchukua mundu kuvuna nafaka.
10 Kisha msherehekee Sikukuu ya Majuma kwa
BWANA Mungu wenu kwa kutoa sadaka ya hiari
kwa kadiri ya baraka ambayo BWANA Mungu
wenu amewapa.
11 Shangilieni mbele za BWANA Mungu wenu
mahali atakapopachagua kama makao ya Jina
lake, ninyi, wana wenu na binti zenu, watumishi
wenu wa kiume na wa kike, Walawi walio katika
miji yenu, na wageni, yatima na wajane waishio
miongoni mwenu.
12 Kumbukeni kwamba mlikuwa watumwa
kule Misri na mfuate amri hizi kwa uangalifu.

### *Sikukuu Ya Vibanda (Walawi 23:33-43)*

13 Adhimisheni sikukuu ya vibanda kwa siku
saba baada ya kukusanya mazao yenu ya nafaka
na kukamua zabibu.
14 Mfurahie sikukuu yenu, ninyi, wana wenu,
binti zenu, watumishi wenu wa kiume na wa
kike, Walawi, wageni, yatima na wajane ambao
wanaishi katika miji yenu.

15 Kwa siku saba mtaiadhimisha sikukuu ya BWANA Mungu wenu katika mahali atakapopachagua BWANA. Kwa kuwa BWANA Mungu wenu atawabariki katika mavuno yenu na katika kazi zote za mikono yenu na furaha yenu itakamilika.

16 Wanaume wenu wote lazima wajitokeze mara tatu kwa mwaka mbele za BWANA Mungu wenu mahali atakapopachagua: kwa ajili ya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, Sikukuu ya Majuma, na Sikukuu ya Vibanda. Hakuna mtu atakayejitokeza mbele za BWANA mikono mitupu:
17 Kila mmoja wenu ni lazima alete zawadi kulingana na jinsi ambavyo BWANA Mungu wenu alivyowabariki.

### *Waamuzi*

18 Wateue waamuzi na maafisa kwa kila kabila lenu katika kila mji ambao BWANA Mungu wenu anawapa, nao watawaamua watu kwa usawa.
19 Msipotoshe haki wala msifanye upendeleo. Msikubali rushwa kwa sababu rushwa hupofusha macho ya wenye busara na kugeuza maneno ya wenye haki.
20 Mfuate haki na haki peke yake, ili mweze kuishi na kuimiliki nchi ambayo BWANA Mungu wenu anawapa.

### *Kuabudu Miungu Mingine*

21 Msisimamishe nguzo yoyote ya Ashera kando ya madhabahu mliyomjengea BWANA Mungu wenu,

22 wala msisimamishe jiwe la kuabudu, kwa
maana BWANA Mungu wenu anavichukia vitu
hivi.

# 17

1 Msimtolee BWANA Mungu wenu dhabihu ya
maksai au kondoo ambaye ana dosari yoyote
au hitilafu ndani yake, kwa kuwa hilo litakuwa
chukizo kwake.
2 Ikiwa mwanaume au mwanamke anayeishi
kati ya mojawapo ya miji akupayo BWANA,
anakutwa anafanya uovu mbele za BWANA
Mungu wenu, kwa kuvunja Agano lake,
3 naye amekwenda kinyume na agizo langu
kuabudu miungu mingine na kuisujudia, kama
vile jua, mwezi au nyota za angani,
4 hili likiwa limeletwa mbele yenu, ni lazima
kulichunguza kikamilifu. Ikiwa ni kweli na
kuwa limehakikishwa kwamba hili ni chukizo
lililofanyika katika Israeli,
5 mchukueni huyo mwanaume au mwanamke
ambaye amelifanya tendo hili ovu kwenye lango
la mji wenu na kumpiga mawe mtu huyo mpaka
afe.
6 Kwa ushuhuda wa mashahidi wawili au
watatu mtu huyo atauawa, bali hakuna mtu
atakayeuawa kwa ushuhuda wa shahidi mmoja
tu.
7 Ni lazima kwanza mikono ya mashahidi
itangulie kumuua huyo mtu, kisha mikono ya
watu wote. Ni lazima mwondoe uovu miongoni
mwenu.

### *Mahakama Za Sheria*

8 Kama mashauri yanaletwa katika mahakama zenu ambayo ni magumu zaidi kwenu kuyaamua, ikiwa ni umwagaji wa damu, madai au mashambulio, yapelekeni mahali ambapo BWANA Mungu wenu atapachagua.
9 Nendeni kwa makuhani, ambao ni Walawi, na kwa mwamuzi ambaye atakuwa kazini wakati huo. Ulizeni kwao nao watawapa maamuzi.
10 Ni lazima mtende sawasawa na maamuzi watakayowapa mahali BWANA atakapopachagua. Kuweni waangalifu kufanya kila kitu watakachowaongoza kufanya.
11 Fanyeni sawasawa na sheria wanayowafundisha na maamuzi wanayowapa. Msigeuke mkono wa kuume au kushoto kuacha kufanya yale wanayowaambia.
12 Mwanaume atakayeonyesha dharau kwa mwamuzi au kwa kuhani ambaye amewekwa kumtumikia BWANA Mungu wenu lazima auawe. Lazima mwondoe uovu katika Israeli.
13 Watu wote watasikia na kuogopa, nao hawatakuwa wenye kudharau tena.

### *Mfalme*

14 Wakati utakapoingia katika nchi anayowapa BWANA Mungu wenu kuimiliki na kukaa humo, nanyi mkasema, “Na tumweke mfalme juu yetu kama mataifa yanayotuzunguka,”
15 kuweni na uhakika wa kumweka mfalme juu yenu ambaye BWANA Mungu wenu atamchagua. Ni lazima atoke miongoni mwa ndugu zenu wenyewe. Msimweke mgeni juu yenu ambaye si ndugu wa Kiisraeli.

16 Hata hivyo, kamwe mfalme asijipatie hesabu
kubwa ya farasi kwa ajili yake mwenyewe, au
kuwafanya watu warudi Misri ili kupata farasi
zaidi, kwa maana BWANA amekuambia, "Ham-
tairudia njia ile tena."
17 Kamwe asioe wake wengi, la sivyo moyo
wake utapotoka. Kamwe asijilimbikizie kiasi
kikubwa cha fedha na dhahabu.
18 Atakapokuwa amekalia kiti cha ufalme
wake, ajiandikie kwenye kitabu nakala ya sheria
kwa ajili yake mwenyewe kutoka zile sheria za
makuhani ambao ni Walawi.
19 Atakuwa na nakala hiyo, naye ataisoma
siku zote za maisha yake ili kwamba ajifunze
kumheshimu BWANA Mungu wake na kufuata
kwa uangalifu maneno yote ya sheria hii na amri
hizi,
20 naye asijifikirie kuwa ni bora kuliko ndugu
zake na kuipotosha sheria. Ndipo yeye na wazao
wake watatawala katika ufalme wake kwa muda
mrefu katika Israeli.

# 18

## *Sadaka Kwa Makuhani Na Walawi*

1 Makuhani ambao ni Walawi, yaani kabila
lote la Lawi, hawatakuwa na mgawo wala urithi
pamoja na Israeli. Wataishi kwa sadaka zitole-
wazo kwa ajili ya BWANA za kuteketezwa kwa
moto, kwa maana huo ndio urithi wao.
2 Hawatakuwa na urithi miongoni mwa ndugu
zao; BWANA ndiye urithi wao, kama alivy-
owaahidi.

3 Hili ndilo fungu la makuhani kutoka kwa
watu watakaotoa dhabihu ya fahali au kondoo:
mguu wa mbele, mataya na matumbo.
4 Mtawapa malimbuko ya nafaka zenu, divai
mpya, mafuta na sufu ya kwanza kutoka many-
oya ya kondoo zenu,
5 kwa kuwa BWANA Mungu wenu amewach-
agua pamoja na wazao wao kutoka makabila
yenu kusimama na kuhudumu katika jina la
BWANA siku zote.
6 Ikiwa Mlawi atahama kutoka mmojawapo ya
miji yenu popote katika Israeli ambapo anaishi,
akaja kwa moyo wote mahali ambapo BWANA
atapachagua,
7 anaweza akahudumu katika jina la BWANA
Mungu wake kama Walawi wenzake wote
wanaohudumu hapo mbele za BWANA.
8 Atashiriki sawa katika mafao yao, hata kama
amepokea fedha kutoka mauzo ya mali ya jamaa
yake.

### *Matendo Ya Machukizo*

9 Wakati mtakapoingia katika nchi ambayo
BWANA Mungu wenu anawapa, msijifunze kuiga
njia za machukizo za mataifa ya huko.
10 Asionekane mtu yeyote miongoni mwenu
ampitishaye mwanawe au binti yake katika
moto, atakayefanya uaguzi, ulozi, anayetabiri
nyakati, anayejishughulisha na uchawi,
11 wala arogaye kwa kupiga mafundo, wala
mwaguzi au anayeabudu mizimu, wala awaom-
baye wafu.

12 Mtu yeyote afanyaye mambo haya ni chukizo kwa BWANA, tena ni kwa sababu ya matendo haya ya kuchukiza wayafanyayo ndiyo maana BWANA Mungu wenu atayafukuza mataifa hayo mbele yenu.
13 Kamwe msilaumiwe mbele za BWANA Mungu wenu.

*Nabii*

14 Mataifa mtakayowafukuza husikiliza wale wafanyao ulozi na uaguzi. Lakini kwenu ninyi, BWANA Mungu wenu hajawaruhusu kufanya hivyo.
15 BWANA Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu wenyewe. Msikilizeni yeye.
16 Kwa kuwa hivi ndivyo mlivyomwomba BWANA Mungu wenu kule Horebu siku ile ya kusanyiko, wakati mliposema, "Na tusiisikie sauti ya BWANA Mungu wetu, wala kuuona moto huu mkubwa tena, ama sivyo tutakufa."
17 BWANA akaniambia: "Wanachosema ni vyema.
18 Nitawainulia nabii kama wewe kutoka miongoni mwa ndugu zao; nitaweka maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia kila kitu nitakachomwamuru.
19 Kama mtu yeyote hatasikiliza maneno yangu ambayo huyo nabii atayasema kwa Jina langu, mimi mwenyewe nitamwajibisha.
20 Lakini nabii ambaye atathubutu kusema kwa Jina langu kitu chochote ambacho sikumwamuru akiseme, au nabii ambaye husema kwa jina la miungu mingine ni lazima auawe."

21 Mnaweza kuulizana wenyewe, "Tutawezaje
kujua wakati ujumbe haukusemwa na BWANA?"
22 Ikiwa kile nabii anachotangaza kwa jina la
BWANA hakikutokea au kutimia, huo ni ujumbe
ambao BWANA hakusema. Nabii huyo amesema
kwa ujuaji. Msimwogope huyo.

# 19

### *Miji Ya Makimbilio*
### *(Hesabu 35:9-34; Yoshua 20:1-9)*

1 Wakati BWANA Mungu wenu atakapokuwa
amewaangamiza mataifa ambayo nchi yao
anawapa ninyi, wakati mtakapokuwa mmewa-
fukuza na kuishi katika miji yao na nyumba zao,
2 ndipo mtenge miji mitatu iliyopo katikati ya
nchi kwa ajili yenu, katika nchi ambayo BWANA
Mungu wenu anawapa kuimiliki.
3 Jengeni barabara katika miji hiyo na kuigawa
mara tatu, nchi anayowapa BWANA Mungu wenu
kama urithi, ili kwamba yeyote amuuaye mtu
aweze kukimbilia humo.
4 Hii ndiyo kanuni kuhusu mtu amuuaye
mwingine na kukimbilia humo kuokoa maisha
yake, yaani, yeye amuuaye jirani yake bila
kukusudia, wala hakumchukia kabla ya hapo.
5 Kwa mfano, mtu aweza kwenda msituni
na jirani yake kukata miti, naye anapozun-
gusha shoka kuangusha mti, shoka linaweza
kuchomoka kutoka kwenye mpini na kumpiga
jirani yake na kumuua. Yule mtu anaweza
kukimbilia katika mmojawapo ya miji hii na
kuokoa maisha yake.

6 Kama sivyo, mlipiza kisasi cha damu anaweza kumfuatilia kwa hasira kali, naye akamkamata na kumuua kama umbali ni mrefu sana hata ingawa hastahili kifo, kwa sababu amemuua jirani yake bila kukusudia.

7 Hii ndiyo sababu nimewaagiza ninyi kutenga miji mitatu ya makimbilio kwa ajili yenu.

8 Kama BWANA Mungu wenu akipanua nchi yenu, kama alivyoahidi kwa kiapo kwa baba zenu na kuwapa nchi yote aliyowaahidi,

9 kwa sababu mmefuata kwa uangalifu sheria zote ninazowaamuru leo, kumpenda BWANA Mungu wenu na kuenenda siku zote katika njia zake, ndipo mtenge miji mingine, mitatu zaidi.

10 Fanyeni hivi ili damu isiyo na hatia isimwagwe katika nchi yenu, ambayo BWANA Mungu wenu anawapa kama urithi wenu, ili kwamba msije mkawa na hatia ya kumwaga damu.

11 Lakini kama mtu anamchukia ndugu yake, akamvizia, akamshambulia na kumuua, kisha akakimbilia katika mmojawapo ya miji hii,

12 wazee wa mji wake watatuma ujumbe kwake, kumleta kutoka mji ule na kumkabidhi mlipiza kisasi cha damu kumuua.

13 Msimwonee huruma. Lazima mwondoe katika Israeli hatia ya umwagaji damu isiyo na hatia ili kwamba mpate kufanikiwa.

14 Usisogeze jiwe la mpaka wa jirani yako ambao uliwekwa na wale waliokutangulia katika urithi upokeao katika nchi BWANA Mungu wako anayowapa kuimiliki.

### *Mashahidi*

15 Shahidi mmoja hatoshi kumtia hatiani mtu
kwa uhalifu au kosa lolote ambalo anaweza
kuwa amelitenda. Lazima shauri lolote
lithibitishwe kwa ushuhuda wa mashahidi
wawili au watatu.
16 Kama shahidi mwenye nia ya kumdhuru
mwingine akisimama kumshtaki mtu kwa uhal-
ifu,
17 watu wawili wanaohusika katika mabishano
lazima wasimame mbele za BWANA na mbele
ya makuhani na waamuzi ambao wako kazini
wakati huo.
18 Waamuzi lazima wafanye uchunguzi kwa
makini na shahidi akionekana kuwa ni mwongo,
akitoa ushuhuda wa uongo dhidi ya ndugu yake,
19 basi mtende kama alivyotaka kumtendea
ndugu yake. Ni lazima mwondoe uovu miongoni
mwenu.
20 Watu watakaosalia watasikia hili na kuo-
gopa, uovu kama huo kamwe hautatendeka tena
miongoni mwenu.
21 Msionyeshe huruma, uhai kwa uhai, jicho
kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono,
mguu kwa mguu.

# 20

*Kwenda Vitani*
1 Mtakapokwenda vitani kupigana na adui
zenu na mkaona farasi na magari ya vita na jeshi
kubwa kuliko lenu, msiwaogope, kwa sababu
BWANA Mungu wenu aliyewatoa kutoka Misri,
atakuwa pamoja nanyi.
2 Wakati mtakapokaribia kwenda vitani,
kuhani atakuja mbele na kuhutubia jeshi.

3 Atasema: "Sikia, ee Israeli, leo unakwenda vitani kupigana na adui zako. Usife moyo wala usiogope, usitishwe wala usitiwe hofu mbele yao.
4 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu ndiye huenda pamoja nanyi kuwapigania dhidi ya adui zenu na kuwapatia ushindi."

5 Maafisa wataliambia jeshi: "Je, kuna yeyote aliyejenga nyumba mpya ambayo haijawekwa wakfu? Yeye na arudi nyumbani, ama sivyo anaweza kufa vitani na mtu mwingine akaiweka wakfu.
6 Je, kuna yeyote aliyepanda shamba la mizabibu na hajaanza kulifurahia? Yeye na arudi nyumbani, au sivyo anaweza kufa vitani na mtu mwingine akalifurahia.
7 Je, kuna yeyote aliyeposa mwanamke na hajamwoa? Yeye na arudi nyumbani, ama sivyo anaweza kufa vitani na mtu mwingine akamwoa."
8 Kisha maafisa wataongeza haya, "Je, kuna mtu anayeogopa ama kufa moyo? Yeye na arudi nyumbani ili ndugu zake nao wasije wakafa moyo pia."
9 Wakati maafisa watakapomaliza kuzungumza na jeshi, watawateua wakuu wa vikosi.
10 Wakati mtakapokwenda kushambulia mji, wapeni watu wake masharti ya amani.
11 Wakikubali na kuwafungulia malango yao, watu wake wote watawatumikia kwa kufanya kazi ngumu na watawatumikia.
12 Ikiwa watakataa kufanya mapatano ya amani na wakiwaingiza katika vita, basi

mtauzunguka mji huo kwa vita.
13 Wakati BWANA Mungu wenu atakapouweka
mji huo mkononi mwenu, waueni kwa upanga
wanaume wote waliomo ndani yake.
14 Kwa upande wa wanawake, watoto, mifugo
na kila kitu kingine chochote ndani ya huo
mji, mnaweza kuvichukua kama nyara kwa ajili
yenu. Nanyi mnaweza kuzitumia hizo nyara
ambazo BWANA Mungu wenu amewapa kutoka
kwa adui zenu.
15 Hivi ndivyo mtakavyofanya kwa miji yote
ambayo iko mbali nanyi, ambayo haimilikiwi na
mataifa ya karibu.
16 Hata hivyo, katika miji ya mataifa ambayo
BWANA Mungu wenu anawapa kama urithi, msi-
ache kitu chochote hai kinachopumua.
17 Waangamizeni kabisa Wahiti, Waamori,
Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wayebusi,
kama BWANA Mungu wenu alivyowaamuru.
18 La sivyo, watawafundisha kufuata mambo
yote ya machukizo wanayofanya wakiabudu
miungu yao, nanyi mtatenda dhambi dhidi ya
BWANA Mungu wenu.
19 Wakati mtakapouzunguka mji kwa vita kwa
muda mrefu, mkipigana dhidi yake ili kuuteka,
msiharibu miti yake kwa kuikata kwa shoka,
kwa sababu mtaweza kula matunda yake. Hivyo
msiikate. Je, miti hiyo ya mashambani ni watu,
hata muizingire?
20 Hata hivyo, mnaweza kuikata miti ambayo
sio miti ya matunda na kuitumia kujenga ngome,
mpaka mji ulio katika vita na ninyi utakapoan-
guka.

# 21

### *Upatanisho Kuhusu Mauaji*

1 Kama mtu akikutwa ameuawa, naye amelala
kwenye shamba katika nchi ambayo BWANA
Mungu wenu anawapa kuimiliki, wala haiju-
likani ni nani aliyemuua,
2 wazee wenu na waamuzi watatoka na
kupima umbali kutoka maiti alipolala mpaka
kwenye miji ya jirani.
3 Kisha wazee wa ule mji ulio karibu zaidi na
yule maiti watamchukua mtamba ambaye ha-
japata kufanyishwa kazi na ambaye hajafungwa
nira,
4 na kumpeleka kwenye bonde ambalo halijap-
ata kulimwa au kupandwa mazao na ambapo
kuna chemchemi itiririkayo. Huko kwenye hilo
bonde, wazee watamvunja yule mtamba shingo.
5 Makuhani, hao wana wa Lawi, wataso-
gea mbele, kwa kuwa BWANA Mungu wenu,
amewachagua kuhudumu na kutoa baraka
katika jina la BWANA, na kuamua mashauri yote
ya mabishano na mashambulio.
6 Ndipo wazee wote wa mji ulio karibu zaidi na
huyo maiti watanawa mikono yao juu ya huyo
mtamba ambaye shingo yake imevunjwa huko
kwenye bonde,
7 nao watatangaza: "Mikono yetu haikumwaga
damu hii, wala macho yetu hayakuona liki-
fanyika.
8 Ee BWANA, ukubali upatanisho kwa watu
wako Israeli, ambao umewakomboa, wala usi-
wahesabie watu wako hatia ya damu ya mtu

asiyekuwa na hatia." Nayo damu iliyomwagika itakuwa imefanyiwa upatanisho.

9 Hivyo mtakuwa mmejitakasa wenyewe kutoka hatia ya kumwaga damu isiyokuwa na hatia, kwa kuwa mmefanya lile lililo sawa mbele za macho ya BWANA.

### *Kuoa Mwanamke Mateka*

10 Mkienda vitani kupigana na adui zenu naye BWANA Mungu wenu akawatia adui mikononi mwenu, nanyi mkachukua mateka,

11 kama ukiona miongoni mwa mateka mwanamke mzuri wa sura nawe wavutwa naye, waweza kumwoa akawa mke wako.

12 Mlete nyumbani mwako, anyoe nywele na kukata kucha zake,

13 avue nguo alizokuwa amevaa alipotekwa. Baada ya kuishi nyumbani mwako na kumwombolezea baba yake na mama yake kwa mwezi mzima, ndipo utakapoweza kumwendea na kuwa mume wake naye atakuwa mke wako.

14 Lakini kama hutaendelea kupendezwa naye, mwache aende popote anapotaka. Kamwe huwezi kumuuza au kumtendea kama mtumwa, kwa sababu utakuwa umemvunjia heshima.

### *Haki Ya Mzaliwa Wa Kwanza*

15 Kama mwanaume ana wake wawili, naye anampenda mmoja na mwingine hampendi na wote wawili wamemzalia wana wa kiume, lakini mwana mzaliwa wa kwanza ni wa yule mke asiyempenda,

16 wakati anapotoa wosia wa mali yake kwa wanawe, kamwe asitoe haki za mzaliwa wa

kwanza kwa mwana wa mke ampendaye kwa upendeleo, badala ya mzaliwa hasa wa kwanza, ambaye ni mwana wa mke ambaye hampendi.
17 Ni lazima amkubali mwana wa mke asiyempenda kama mzaliwa wa kwanza kwa kumpa sehemu ya vile vyote alivyo navyo maradufu. Mwana huyo ni ishara ya kwanza ya nguvu za baba yake. Haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake yeye.

### *Mwana Mwasi*

18 Kama mtu ana mwana mkaidi na mwasi ambaye hamtii baba yake na mama yake, na hasikii wazazi wanapomrudi,
19 baba yake na mama yake watamleta kwa wazee kwenye lango la mji wake.
20 Watawaambia wazee, “Huyu mwanetu ni mkaidi na mwasi. Hatutii sisi, yeye ni mpotovu na mlevi.”
21 Kisha wanaume wote wa mjini mwake watampiga kwa mawe mpaka afe. Ndivyo imewapasa kuondoa maovu kati yenu. Israeli yote itasikia hili na kuogopa.

### *Sheria Mbalimbali*

22 Kama mtu ana hatia ya kosa linalompasa kuuawa naye akauawa, mwili wake utaangikwa mtini,
23 kamwe msiuache mwili wake mtini usiku kucha. Hakikisheni mnauzika mwili wake siku ile ile, kwa sababu kila mtu anayeangikwa mtini yupo chini ya laana ya Mungu. Msiinajisi nchi ambayo BWANA Mungu wenu anawapa kama urithi wenu.

# 22

1 Kama ukimwona ng'ombe au kondoo wa
ndugu yako anapotea, usipuuze, bali uhakikishe
unamrudisha kwa mwenyewe.
2 Ikiwa huyo ndugu haishi karibu nawe au
kama hufahamu yeye ni nani, mchukue nyum-
bani kwako huyo mnyama umweke mpaka
mwenyewe aje kumtafuta. Ndipo umrudishie.
3 Fanya vivyo hivyo ukimkuta punda wa
nduguyo au joho lake au chochote alichopoteza.
Usipuuze jambo hilo.
4 Kama ukimwona punda wa nduguyo au
ng'ombe wake ameanguka barabarani, usipuuze
jambo hilo. Msaidie asimame kwa miguu yake.
5 Haimpasi mwanamke kuvaa nguo za kiume
wala mwanaume kuvaa nguo za kike, kwa
maana Bwana Mungu wenu anachukia yeyote
ambaye hufanya hivi.
6 Kama ukikuta kiota cha ndege kando ya
barabara, iwe juu ya mti au chini, naye ndege
amelala juu ya makinda au mayai, usimchukue
huyo ndege pamoja na makinda yake.
7 Waweza kuchukua makinda, lakini uwe na
hakika ya kumwacha huyo ndege, ili upate
kufanikiwa na uweze kuishi maisha marefu.
8 Wakati unapojenga nyumba mpya, fanya
ukuta wa kuzuia kandokando ya dari ili usijiletee
hatia ya kumwaga damu juu ya nyumba yako
ikiwa yeyote ataanguka kutoka humo.
9 Usipande aina mbili za mbegu katika shamba
lako la mizabibu; ikiwa utafanya hivyo, si mazao
utakayopanda tu yatakuwa najisi, bali nayo
matunda ya shamba la mizabibu pia.

10 Usilime kwa maksai aliyefungwa nira pamoja na punda.
11 Usivae nguo za sufu na kitani zilizofumwa pamoja.
12 Fanya vishada kwenye pembe nne za joho unalovaa.

### *Kukiuka Taratibu Za Ndoa*

13 Ikiwa mtu atamwoa mke na, baada ya kufanya naye tendo la ndoa, akamchukia,
14 akimsingizia na kumwita jina baya, akisema, “Nilimwoa mwanamke huyu, lakini nilipomkaribia sikupata uthibitisho wa ubikira wake”
15 ndipo baba na mama wa msichana wataleta uthibitisho kwamba alikuwa bikira kwa wazee wa mji kwenye lango.
16 Baba wa msichana atawaambia wazee, “Nilimwoza binti yangu kwa huyu mwanaume, lakini hampendi.
17 Sasa amemsingizia na kusema, ‘Sikumkuta huyu binti akiwa bikira.’ Lakini hapa kuna uthibitisho wa ubikira wa binti yangu.” Kisha wazazi wake wataonyesha nguo zake kwa wazee wa mji,
18 nao wazee watamchukua huyo mwanaume na kumwadhibu.
19 Watamtoza shekeli mia moja* za fedha na kupewa wazazi wa msichana, kwa sababu mwanaume huyu amempa bikira wa Kiisraeli jina baya. Ataendelea kuwa mke wake; kamwe hawezi kumpa talaka siku zote za maisha yake.

---

* **22:19** Shekeli 100 za fedha ni sawa na kilo moja.

20 Hata hivyo, kama shtaka ni la kweli na
hakuna uthibitisho juu ya ubikira wa huyo
msichana ulioweza kupatikana,
21 huyo msichana ataletwa kwenye mlango wa
nyumba ya baba yake, na hapo watu wa mji
wake watampiga kwa mawe hadi afe. Amefanya
kitu cha aibu katika Israeli kwa kufanya ukahaba
akiwa nyumbani kwa babaye. Lazima mwondoe
uovu katikati yenu.
22 Ikiwa mwanaume atakutwa akizini na mke
wa mtu mwingine, wote wawili, mwanaume
na mwanamke aliyezini naye, lazima wauawe.
Lazima mwondoe uovu katika Israeli.
23 Ikiwa mwanaume atakutana na bikira mjini
ambaye ameposwa na mtu akazini naye,
24 utawachukua wote wawili kwenye lango la
mji na kuwapiga kwa mawe mpaka wafe; yule
msichana kwa kuwa alikuwa mjini na hakupiga
kelele kuomba msaada, na yule mwanaume kwa
sababu amemtenda jeuri mke wa mtu mwingine.
Lazima mwondoe uovu katikati yenu.
25 Lakini ikiwa itatokea mwanaume akaku-
tana na msichana aliyeposwa huko masham-
bani, akambaka, mwanaume aliyefanya hivi
peke yake ndiye atakayeuawa.
26 Usimtendee msichana yule jambo lolote;
hajafanya dhambi inayostahili kifo. Shauri hili
ni kama lile la yeyote ambaye anamshambulia
na kumuua kwa makusudi jirani yake,
27 kwa maana mwanaume huyo alimkuta
msichana huko mashambani, na ingawa
msichana aliyeposwa alipiga kelele, hapakuwa
na mtu wa kumwokoa.

28 Ikiwa itatokea mwanaume akutane na bikira ambaye hajaposwa na kumbaka nao wakakutwa,
29 mwanaume atamlipa baba wa msichana shekeli hamsini† za fedha. Ni lazima amwoe huyo msichana, kwa maana amemfanyia jeuri. Kamwe hawezi kumpa talaka siku zote za maisha yake.
30 Mwanaume asimwoe mke wa baba yake; kamwe asidhalilishe kitanda cha baba yake.

# 23

*Kutengwa Na Mkutano*

1 Asiingie mtu yeyote aliyehasiwa kwa kupondwa makende au kwa kukatwa uume wake katika kusanyiko la BWANA.
2 Mtu yeyote ambaye amezaliwa kwenye ndoa isiyo halali au wazao wake wasiingie kwenye kusanyiko la BWANA, hata mpaka kizazi cha kumi.
3 Hapatakuwa na Mwamoni au Mmoabu au yeyote wa wazao wao atakayeruhusiwa kuingia katika kusanyiko la BWANA, hata mpaka kizazi cha kumi.
4 Kwa kuwa hawakuja kuwalaki wakiwa na mkate na maji mlipokuwa njiani mlipotoka Misri, tena walimwajiri Balaamu mwana wa Beori kutoka Pethori iliyoko Aramu-Naharaimu* ili kuwalaani ninyi.
5 Hata hivyo, BWANA Mungu wenu hakumsikiliza Balaamu bali aligeuza laana kuwa

† **22:29** Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600. * **23:4** Yaani Mesopotamia ya Kaskazini-Magharibi.

baraka kwenu kwa sababu BWANA Mungu wenu anawapenda.

6 Msitafute mapatano ya urafiki nao maisha yenu yote.

7 Usimchukie Mwedomu, kwa kuwa yeye ni ndugu yako. Usimchukie Mmisri, kwa sababu uliishi kama mgeni katika nchi yake.

8 Kizazi cha tatu cha watoto watakaozaliwa nao wanaweza kuingia katika kusanyiko la BWANA.

### *Unajisi Katika Kambi*

9 Unapokuwa umepiga kambi dhidi ya adui zako, jitenge na kitu chochote kisicho safi.

10 Ikiwa mtu amechafuka kwa sababu ya kutokwa na shahawa usiku, inampasa atoke nje ya kambi na kukaa huko.

11 Lakini jioni ikikaribia ataoga, na baada ya jua kuzama ataingia tena kambini.

12 Tengeni mahali nje ya kambi ambapo mnaweza kwenda kujisaidia.

13 Kama sehemu ya vifaa vyenu kuweni na kitu cha kulimia, nanyi mnapojisaidia, chimba shimo na kisha funika kile kikutokacho.

14 Kwa kuwa BWANA Mungu wenu hutembea katika kambi yenu ili kuwalinda na kuwaweka adui zenu mikononi mwenu. Kambi yenu ni lazima iwe takatifu, ili asione kitu chochote miongoni mwenu kilicho kichafu akageuka na kuwaacha.

### *Sheria Mbalimbali*

15 Ikiwa mtumwa amekimbilia kwako, usimrudishe kwa bwana wake.

16 Mwache aishi miongoni mwenu mahali
popote anapopapenda na katika mji wowote
anaochagua. Usimwonee.

17 Asiwepo Mwisraeli mwanamke kahaba au
mwanaume hanithi wa mahali pa kuabudia
miungu.
18 Kamwe usilete mapato ya ukahaba ikiwa
ni ya mwanamke au ni ya mwanaume katika
nyumba ya BWANA Mungu wako kwa ajili ya
nadhiri yoyote, kwa sababu BWANA Mungu wako
anachukizwa na yote mawili.

19 Usimtoze ndugu yako riba, iwe ni fedha ama
chakula ama kitu kingine chochote ambacho
waweza kupata riba juu yake.
20 Unaweza kumtoza mgeni riba, lakini siyo
nduguyo Mwisraeli, ili kwamba BWANA Mungu
wako akubariki katika kila kitu unachoweka
mkono katika nchi unayoingia kuimiliki.

21 Ukiweka nadhiri kwa BWANA Mungu wako,
usichelewe kuitimiza, kwa kuwa BWANA Mungu
wako atakudai, nawe utakuwa na hatia ya
dhambi.
22 Lakini ukijizuia kuweka nadhiri, hutakuwa
na hatia.
23 Chochote kitakachotamkwa kwa midomo
yako ni lazima uhakikishe umekifanya, kwa
sababu uliweka nadhiri yako kwa hiari mbele
za BWANA Mungu wako kwa kinywa chako
mwenyewe.

24 Kama ukiingia katika shamba la mizabibu
la jirani yako, unaweza kula zabibu kadiri
utakavyo, lakini usiweke chochote kwenye
kikapu chako.

25 Kama ukiingia katika shamba la nafaka la
jirani yako, unaweza kukwanyua kwa mikono
yako, lakini usikate kwa mundu nafaka iliyosi-
mama.

# 24

### *Sheria Kuhusu Ndoa Na Talaka*

1 Ikiwa mtu atamwoa mke na akamchukia kwa
sababu ya kukosa adabu, naye akamwandikia
hati ya talaka, akampa na kumfukuza kutoka
nyumbani kwake,
2 ikiwa baada ya kuondoka nyumbani kwake
atakuwa mke wa mtu mwingine,
3 ikiwa mume wake wa pili atachukizwa naye
akamwandikia hati ya talaka, akampa na kum-
fukuza kutoka nyumbani kwake, au kama akifa,
4 basi yule mume wake wa kwanza, ambaye
alimpa talaka, haruhusiwi kumwoa tena baada
ya mwanamke huyo kuwa najisi. Hayo
yatakuwa machukizo machoni pa BWANA.
Usilete dhambi juu ya nchi ambayo BWANA
Mungu wako anakupa kama urithi.
5 Kama mtu ameoa karibuni, kamwe
asipelekwe vitani au kupewa wajibu mwingine
wowote. Kwa mwaka mmoja atakuwa
huru kubaki nyumbani ili amfurahishe mke
aliyemwoa.
6 Usitoe jozi ya mawe ya kusagia, hata ikiwa
lile la juu, kuweka rehani kwa ajili ya deni, kwa
sababu itakuwa ni kuweka uhai wa mtu kama
dhamana.
7 Kama mtu akikamatwa akiiba yeyote mion-
goni mwa ndugu zake wa Waisraeli na kumtenda

kama mtumwa au akimuuza, mwizi huyo ni lazima auawe. Nawe utaondoa uovu kutoka miongoni mwenu.

8 Pakitokea magonjwa ya ngozi ya kuambukiza, mwe waangalifu sana kufanya sawasawa na maagizo ya makuhani, ambao ni Walawi. Ni lazima mfuate kwa uangalifu yale niliyowaamuru.
9 Kumbukeni kile BWANA Mungu wenu alichomfanyia Miriamu njiani baada ya ninyi kutoka Misri.
10 Unapomkopesha jirani yako chochote, usiingie nyumbani kwake kutwaa kile anachokitoa kama rehani.
11 Ukae nje na umwache huyo mtu uliyemkopesha akuletee hiyo rehani.
12 Ikiwa mtu huyo ni maskini, usiende kulala ukiwa na hiyo rehani yake katika milki yako.
13 Rudisha vazi lake kabla ya machweo ya jua ili apate kulilalia. Kisha atakushukuru na kitaonekana kama kitendo cha haki mbele za BWANA Mungu wako.

14 Usimwonee mtu maskini na mhitaji ambaye umemwajiri, akiwa ni nduguyo Mwisraeli au mgeni anayeishi katika mojawapo ya miji yenu.
15 Mlipe ujira wake kila siku kabla ya jua kutua, kwa sababu yeye ni maskini na anautegemea ujira huo. La sivyo, anaweza kumlilia BWANA dhidi yako, nawe ukapata hatia ya dhambi.
16 Baba wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mmoja atakufa kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.

17 Usipotoshe hukumu ya mgeni au yatima, au
kuchukua vazi la mjane kama rehani.
18 Kumbukeni kwamba mlikuwa watumwa
huko Misri, naye BWANA Mungu wenu
akawakomboa kutoka huko. Hii ndiyo sababu
ninawaamuru kutenda hili.
19 Unapovuna shamba lako na ukasahau
mganda, usirudi kuuchukua. Acha kwa ajili
ya mgeni, yatima na mjane, ili BWANA Mungu
wako aweze kukubariki wewe katika kazi zote
za mikono yako.
20 Unapovuna zeituni kutoka miti yako,
usirudie matawi mara ya pili. Acha kilichobaki
kwa ajili ya mgeni, yatima na mjane.
21 Unapochuma zabibu katika shamba lako la
mizabibu usirudie tena. Acha zinazobaki kwa
ajili ya mgeni, yatima na mjane.
22 Kumbuka kwamba mlikuwa watumwa
katika nchi ya Misri. Ndiyo sababu ninawaa-
muru kufanya hili.

# 25

1 Watu wanapokuwa na ugomvi, wapeleke ma-
hakamani na waamuzi wataamua shauri hilo;
watawaachia wasio na kosa na kuwahukumu
wenye hatia.
2 Kama mtu mwenye hatia anastahili
kuchapwa, mwamuzi atamwamuru alale
chini ili achapwe mbele yake idadi ya viboko
kulingana na kosa lake,
3 lakini kamwe asichapwe zaidi ya viboko
arobaini. Ikiwa atachapwa zaidi ya viboko
arobaini, nduguyo atadhalilika machoni pako.

4 Usimfunge maksai kinywa anapopura
nafaka.

5 Ikiwa ndugu wanaishi pamoja na mmoja wao
akafa bila kuacha mwana, kamwe mjane wake
asiolewe nje ya jamaa hiyo. Ndugu wa mumewe
atamchukua, amwoe na kutimiza wajibu wa
shemeji kwake.
6 Mwana wa kwanza atakayemzaa atapewa
jina la ndugu aliyekufa ili jina lake lisifutike
katika Israeli.

7 Hata hivyo, ikiwa ndugu huyo wa mume
hataki kuoa huyo mke wa nduguye, mjane
atawaendea wazee kwenye lango la mji na
kusema, “Ndugu wa mume wangu anakataa
kuendeleza jina la nduguye katika Israeli. Hataki
kutimiza wajibu wa shemeji kwangu.”
8 Ndipo wazee wa mji wake watamwita na
kuzungumza naye. Kama atashikilia kukataa
akisema, “Sitaki kumwoa,”
9 mjane wa nduguye atamwendea mbele ya
wazee, atamvua kiatu kimoja na kumtemea
mate usoni, na kusema, “Hivi ndivyo ambavyo
hufanywa kwa mtu ambaye atakataa kuendeleza
jamaa ya ndugu yake.”
10 Jamaa ya mtu huyo itafahamika katika
Israeli kama Jamaa ya Aliyevuliwa Kiatu.

11 Ikiwa watu wawili wanapigana na mke wa
mmoja wao akaja kumwokoa mumewe na yule
anayemshambulia, naye mke huyo akifika na
kumkamata sehemu za siri,
12 huyo mwanamke utamkata mkono wake.
Usimhurumie.

13 Usiwe na mawe ya kupimia ya aina mbili
katika mkoba wako, moja zito na jingine jepesi.
14 Usiwe na vipimo viwili tofauti katika
nyumba yako, kimoja kikubwa, kingine kidogo.
15 Ni lazima uwe na uzito na vipimo sahihi na
vya haki, ili upate kuishi maisha marefu katika
nchi anayokupa BWANA Mungu wako.
16 Kwa maana BWANA Mungu wako humchukia
yeyote ambaye hufanya mambo kama haya,
yeyote anayetenda kwa udanganyifu.
17 Kumbuka kile Waamaleki walichowatendea
mlipokuwa njiani mkitoka Misri.
18 Wakati mlipokuwa mmechoka na kuishiwa
nguvu kwa safari yenu, wakawapiga wale wote
waliokuja nyuma. Waamaleki hawakumwogopa
Mungu.
19 BWANA Mungu wako atakapokupa pumziko
mbali na adui zako wote wanaokuzunguka
katika nchi akupayo kuimiliki kuwa urithi, utafutilia mbali kumbukumbu lote la Waamaleki
chini ya mbingu. Usisahau!

# 26

*Malimbuko Na Zaka*

1 Mtakapokuwa mmeingia nchi ile ambayo
BWANA Mungu wenu anawapa kama urithi na
mtakapokuwa mmeimiliki na kukaa ndani yake,
2 chukueni baadhi ya mavuno ya kwanza ya
yale yote mtakayozalisha kutoka udongo wa
nchi ambayo BWANA Mungu wenu anawapa na
mweke kwenye kapu. Kisha uende mahali
ambapo BWANA Mungu wako atapachagua kuwa
makao kwa ajili ya Jina lake

3 na umwambie kuhani atakayekuwepo kwa
wakati huo, “Ninatangaza leo kwa BWANA
Mungu wako kwamba nimekuja katika nchi
ambayo BWANA aliwaapia baba zetu kwamba
atatupa.”
4 Kuhani atapokea lile kapu mikononi mwako
na kuliweka chini mbele ya madhabahu ya
BWANA Mungu wako.
5 Kisha utatangaza mbele za BWANA Mungu
wako: “Baba yangu alikuwa Mwaramu
aliyekuwa anatangatanga, akaenda Misri
pamoja na watu wachache, akaishi huko hadi
akawa taifa kubwa, lenye nguvu na watu wengi.
6 Lakini Wamisri walituonea na kututaabisha,
wakitufanyisha kazi ngumu.
7 Kisha tulimlilia BWANA, Mungu wa baba
zetu, naye BWANA akasikia sauti yetu na akaona
huzuni yetu, taabu yetu na mateso yetu.
8 Kwa hiyo BWANA akatutoa nchi ya Misri kwa
mkono wenye nguvu na ulionyooshwa, pamoja
na utisho mkuu, ishara za miujiza na maajabu.
9 Akatuleta mahali hapa akatupa nchi hii, nchi
inayotiririka maziwa na asali;
10 nami sasa ninaleta malimbuko ya ardhi
ambayo wewe, Ee BWANA, umenipa.” Weka kapu
mbele za BWANA Mungu wako na usujudu mbele
zake.
11 Kisha wewe pamoja na Walawi na wageni
wote walioko miongoni mwenu mtafurahi katika
vitu vyote vizuri ambavyo BWANA Mungu wenu
amewapa pamoja na wa nyumbani mwenu.
12 Wakati utakapokuwa umeshatoa zaka zote
za mazao yako katika mwaka wa tatu, ambao ni

mwaka wa zaka, utampa Mlawi, mgeni, yatima
na mjane, ili waweze kula katika miji yenu na
kushiba.
13 Kisha umwambie BWANA Mungu wako:
"Nimeondoa katika nyumba yangu ile sehemu
iliyowekwa wakfu na nimempa Mlawi, mgeni,
yatima na mjane, kulingana na yote uliyoamuru.
Sijazihalifu amri zako wala kusahau hata mo-
jawapo.
14 Sijala sehemu iliyowekwa wakfu wakati
nilipokuwa nikiomboleza, wala sijaondoa mo-
jawapo wakati nilipokuwa najisi, wala sijatoa
sehemu yake yoyote kwa wafu. Nimemtii BWANA
Mungu wangu; nimefanya kila kitu ulichonia-
muru.
15 Angalia chini kutoka mbinguni, maskani
yako matakatifu, uwabariki watu wako Israeli
pamoja na nchi uliyotupa kama ulivyoahidi kwa
kiapo kwa baba zetu, nchi inayotiririka maziwa
na asali."

## *Fuata Maagizo Ya BWANA*

16 BWANA Mungu wako anakuagiza leo kufuata
amri hizi na sheria; zishike kwa bidii kwa moyo
wako wote na kwa roho yako yote.
17 Umetangaza leo kwamba BWANA ndiye
Mungu wako na kwamba utafuata njia zake,
kwamba utayashika maagizo yake, amri zake na
sheria zake nawe utamtii.
18 Naye BWANA ametangaza leo kwamba ninyi
ni taifa lake, hazina yake ya thamani kama
alivyoahidi, ili kwamba mpate kuyashika maa-
gizo yake yote.

19 Ametangaza kwamba atawaweka juu kuliko mataifa mengine aliyoyafanya katika sifa, kuwa fahari na heshima, na kwamba mtakuwa taifa takatifu kwa BWANA Mungu wenu, kama alivyoahidi.

# 27

## *Madhabahu Katika Mlima Ebali*

1 Mose na wazee wa Israeli wakawaagiza watu: "Yashikeni maagizo haya yote ninayowaagiza leo.
2 Mtakapokuwa mmevuka Mto Yordani na kuingia katika nchi awapayo BWANA Mungu wenu, msimamishe mawe makubwa na mkayatie lipu.
3 Andikeni juu yake maneno yote ya sheria hii wakati mtakapokuwa mmevuka na kuingia katika nchi awapayo BWANA Mungu wenu, nchi itiririkayo maziwa na asali, kama vile BWANA, Mungu wa baba zenu, alivyowaahidi.
4 Mtakapokuwa mmevuka Yordani, simamisheni mawe haya juu ya Mlima Ebali, kama ninavyowaagiza leo, mkayatie lipu.
5 Huko mjengeeni BWANA Mungu wenu madhabahu, madhabahu ya mawe. Msitumie kifaa chochote cha chuma juu yake.
6 Jengeni madhabahu ya BWANA Mungu wenu kwa mawe ya shambani, na mtoe sadaka za kuteketezwa juu yake kwa BWANA Mungu wenu.
7 Toeni sadaka za amani juu yake, mkizila na kufurahia mbele za BWANA Mungu wenu.

8 Nanyi mtaandika maneno yote ya sheria
hii kwa wazi sana juu ya mawe haya ambayo
mmesimamisha."

### *Laana Kutoka Mlima Ebali*

9 Kisha Mose na makuhani, ambao ni Walawi,
wakawaambia Israeli wote, "Nyamaza ee Israeli,
sikiliza! Sasa umekuwa taifa la BWANA Mungu
wako.
10 Mtii BWANA Mungu wako, na kufuata amri
zake na maagizo ninayokupa leo."
11 Siku ile ile Mose akawaagiza watu:
12 Mtakapovuka Mto Yordani, makabila haya
yatasimama juu ya Mlima Gerizimu kubariki
watu: Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, Yosefu na
Benyamini.
13 Makabila haya yatasimama juu ya Mlima
Ebali kwa kutamka laana: Reubeni, Gadi, Asheri,
Zabuloni, Dani na Naftali.
14 Nao Walawi watawasomea watu wote wa
Israeli kwa sauti kubwa:
15 "Alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya ku-
chonga au mwenye kusubu sanamu, kitu am-
bacho ni chukizo kwa BWANA, kazi ya mikono
ya fundi stadi, na kuisimamisha kwa siri."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
16 "Alaaniwe mtu amdharauye baba yake na
mama yake."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
17 "Alaaniwe mtu asogezaye jiwe la mpaka
wa jirani yake."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
18 "Alaaniwe mtu ampotoshaye kipofu
njiani."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"
19 "Alaaniwe mtu apotoshaye haki ya mgeni,
yatima au mjane."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
20 "Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na mke
wa baba yake, kwa maana anadharau malazi
ya baba yake."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
21 "Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na
mnyama yeyote."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
22 "Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na dada
yake, binti wa baba yake au binti wa mama
yake."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
23 "Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na
mama mkwe wake."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
24 "Alaaniwe mtu amuuaye jirani yake kwa
siri."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
25 "Alaaniwe mtu apokeaye rushwa ili ku-
muua mtu asiye na hatia."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"
26 "Alaaniwe mtu yule ambaye hatashikilia
maneno ya sheria hii kwa kuyatekeleza."
Kisha watu wote watasema, "Amen!"

# 28

*Baraka Za Utiifu*
*(Walawi 26:3-13; Kumbukumbu 7:12-24)*

1 Kama ukimtii BWANA Mungu wako kwa bidii
na kufuata amri zake zote ninazokupa leo kwa

bidii, BWANA Mungu wako atakuweka juu ya mataifa yote katika dunia.

2 Baraka hizi zote zitakuja juu yako na kukupata, kama ukimtii BWANA Mungu wako:

3 Utabarikiwa mjini na utabarikiwa mashambani.

4 Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na mazao ya nchi yako na wanyama wako wachanga wa kufugwa, yaani ndama wa makundi yako ya ng'ombe, na wana-kondoo wa makundi yako.

5 Kapu lako na vyombo vyako vya kukandia vitabarikiwa.

6 Utabarikiwa uingiapo na utabarikiwa utokapo.

7 BWANA atasababisha adui wainukao dhidi
yako kushindwa mbele yako. Watakujia kwa njia moja lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.

8 BWANA ataagiza baraka juu ya ghala zako na juu ya kila kitu utakachogusa kwa mkono wako. BWANA Mungu wako atakubariki katika nchi anayokupa.

9 BWANA atakufanya kuwa taifa lake takatifu, kama alivyokuahidi kwa kiapo, kama ukishika maagizo ya BWANA Mungu wako na kwenda katika njia zake.

10 Kisha mataifa yote ya dunia wataona kuwa unaitwa kwa jina la BWANA, nao watakuogopa.

11 BWANA atakupa kustawi kwa wingi, katika tunda la uzao wa tumbo lako, katika wanyama wachanga wa mifugo yako na katika mazao ya

ardhi yako, katika nchi aliyowaapia baba zako
kuwapa.

12 BWANA atafungua mbingu, ghala zake
za baraka, kukupa mvua kwa majira yake
na kubariki kazi zako zote za mikono yako.
Utakopesha mataifa mengi lakini hutakopa kwa
yeyote.
13 BWANA atakufanya kichwa, wala si mkia.
Kama utazingatia maagizo ya BWANA Mungu
wako ninayokupa siku hii ya leo na kuyafuata
kwa bidii, daima utakuwa juu, kamwe hutakuwa
chini.
14 Usihalifu amri zangu zozote ninazokupa leo,
kwa kwenda kuume au kushoto, kwa kufuata
miungu mingine na kuitumikia.

### *Laana Kwa Kutokutii*
### *(Walawi 26:14-46)*

15 Hata hivyo, kama hutamtii BWANA Mungu
wako na kuzishika kwa bidii amri zake zote na
maagizo ninayokupa leo, laana hizi zote zitakuja
juu yako na kukupata:

16 Utalaaniwa mjini na utalaaniwa mashambani.

17 Kapu lako na chombo chako cha kukandia kitalaaniwa.

18 Uzao wa tumbo lako utalaaniwa, mazao ya ardhi yako, ndama wa makundi yako ya ng'ombe na wana-kondoo wa makundi yako.

19 Utalaaniwa uingiapo na utokapo.

20 BWANA ataleta laana juu yako, fadhaa
na kukaripiwa katika kila kitu unachokigusa
kwa mkono wako, mpaka uwe umeharibiwa

na kuangamizwa ghafula kwa ajili ya maovu uliyoyafanya kwa kumwacha yeye.

21 BWANA atakupiga kwa magonjwa mpaka akuangamize kutoka nchi unayoingia kuimiliki.

22 BWANA atakupiga kwa magonjwa ya kudhoofisha, kwa homa na kuwashwa, hari na kwa ukame, kutu na kuwa na uchungu ambavyo vitakupiga mpaka uangamie.

23 Anga juu yako itakuwa shaba, na ardhi chini yako itakuwa chuma.

24 BWANA atafanya mvua ya nchi yako kuwa mavumbi na mchanga; vitakujia kutoka angani mpaka uangamie.

25 BWANA atakufanya ushindwe mbele ya adui zako. Utawajia kwa njia moja lakini utawakimbia mbele yao kwa njia saba, nawe utakuwa kitu cha kuchukiza kwa falme zote za dunia.

26 Mizoga yenu itakuwa chakula cha ndege wa angani na wanyama wa nchi, wala hapatakuwepo mtu yeyote wa kuwafukuza.

27 BWANA atakupiga kwa majipu ya Misri na kwa vidonda vitokavyo usaha na kuwashwa, ambako huwezi kuponywa.

28 BWANA atakupiga kwa wazimu, upofu na kuchanganyikiwa kwa akili.

29 Wakati wa adhuhuri utapapasapapapasa huku na huko kama mtu kipofu katika giza. Hutafanikiwa katika lolote ufanyalo; siku baada ya siku utaonewa na kunyang'anywa, wala hakuna yeyote atakayekuokoa.

30 Utaposa mke, lakini mtu mwingine atakutana naye kimwili. Utajenga nyumba, lakini

hutaishi ndani yake. Utapanda shamba la mizabibu, lakini hutakula matunda yake.

31 Ng'ombe wako atachinjwa mbele ya macho yako lakini hutakula nyama yake. Punda wako atachukuliwa kwa nguvu kutoka kwako wala hatarudishwa. Kondoo wako watapewa adui zako, wala hakuna mtu yeyote wa kuwaokoa.

32 Wanao na binti zako watatolewa kwa mataifa mengine, nawe utayachosha macho yako ukiwatazamia siku baada ya siku, hutakuwa na nguvu kuinua mkono.

33 Taifa usilolijua watakula mazao ya nchi yako na taabu ya kazi yako, hutakuwa na chochote, bali kuonewa kikatili siku zako zote.

34 Vitu utakavyoviona kwa macho yako vitakufanya wazimu.

35 BWANA atayapiga magoti yako na miguu yako kwa majipu yenye maumivu makali yasiyoponyeka, yakienea kutoka nyayo za miguu yako hadi utosini.

36 BWANA atakupeleka wewe na mfalme uliyemweka juu yako uende kwenye taifa ambalo hukulijua wewe wala baba zako. Huko utaabudu miungu mingine, miungu ya miti na mawe.

37 Utakuwa kitu cha kuchukiza, tena kitu cha kudharauliwa na kudhihakiwa kwa mataifa yote huko BWANA atakakokupeleka.

38 Utapanda mbegu nyingi katika shamba lakini utavuna haba, kwa sababu nzige watazila.

39 Utapanda mashamba ya mizabibu na kuyapalilia, lakini hutakunywa divai yake wala

hutakusanya zabibu, kwa sababu wadudu
watazila.
40 Utakuwa na mizeituni katika nchi yako yote,
lakini hutatumia hayo mafuta yake, kwa sababu
zeituni zitapukutika.
41 Utakuwa na wana na binti lakini
hawatakuwa nawe, kwa sababu watachukuliwa
mateka.
42 Makundi ya nzige yatavamia miti yako yote
na mazao ya nchi yako.
43 Mgeni anayeishi miongoni mwako atainuka
juu zaidi na zaidi kuliko wewe, lakini wewe
utashuka chini zaidi na zaidi.
44 Yeye atakukopesha, lakini wewe hutamkope-
sha. Yeye atakuwa kichwa, lakini wewe utakuwa
mkia.
45 Laana hizi zote zitakuja juu yako. Zi-
takufuatia na kukupata mpaka uangamizwe,
kwa sababu hukumtii BWANA Mungu wako, na
kuzishika amri zake na maagizo yake aliyokupa.
46 Zitakuwa ishara na ajabu kwako na kwa
wazao wako milele.
47 Kwa sababu hukumtumikia BWANA Mungu
wako kwa furaha na kwa moyo wakati wa
kufanikiwa kwako,
48 kwa hiyo katika njaa na kiu, katika uchi na
umaskini wa kutisha, utawatumikia adui ambao
BWANA atawatuma dhidi yako. Yeye ataweka
nira ya chuma shingoni mwako hadi amekwisha
kukuangamiza.
49 BWANA ataleta taifa dhidi yako kutoka mbali,
kutoka miisho ya dunia, kama tai ashukiavyo
mawindo chini, taifa ambalo hutaijua lugha
yake,

50 taifa lenye uso mkali lisilojali wazee wala
kuwahurumia vijana.
51 Watakula wadogo wa mifugo yako na
mazao ya nchi yako mpaka umeangamia.
Hawatakuachia nafaka, divai mpya au mafuta,
wala ndama wowote wa kundi lako au wana-
kondoo wa kundi lako mpaka umekuwa magofu.
52 Nao wataizingira miji yote katika nchi yako
mpaka kuta ndefu za ngome ambazo unazitege-
mea zimeanguka. Watazingira miji yote katika
nchi ambayo BWANA Mungu wako anakupa.

53 Utakula uzao wa tumbo lako, nyama ya
wana wako na binti zako ambao BWANA Mungu
wako amekupa, kwa sababu ya mateso yale adui
zako watakayokuletea wakati wa kukuzingira.
54 Hata yule mtu muungwana sana na makini
miongoni mwako hatakuwa na huruma kwa
ndugu yake mwenyewe au kwa mke ampendaye
au watoto wake waliosalia,
55 naye hatampa hata mmoja wao nyama ya
watoto wake ambao anawala. Kwa kuwa hakuna
kitu kingine kilichosalia kwake katika mazin-
girwa makali ambayo adui yako watakuletea
kwa miji yako yote.
56 Mwanamke ambaye ni muungwana sana
na makini miongoni mwako, yaani ambaye
ni makini sana na muungwana kiasi kwamba
asingethubutu kugusa ardhi kwa wayo wa mguu
wake, yeye atakuwa mchoyo kwa mume ampen-
daye na mwanawe mwenyewe au binti yake,
57 kondoo wa nyuma kutoka kwenye tumbo
lake na watoto anaowazaa. Kwa kuwa anakusu-
dia kuwala kwa siri wakati wa kuzingirwa na

katika taabu zile ambazo adui yako atazileta juu
yako na miji yako.

58 Kama hutafuata kwa bidii maneno yote ya
sheria hii, ambayo yameandikwa katika kitabu
hiki na kama hutalicha hili jina la fahari na la
kutisha, yaani la BWANA Mungu wako,
59 BWANA ataleta mapigo ya kutisha juu yako
na kwa wazao wako, maafa makali na ya
kudumu, magonjwa mazito na ya kudumu.
60 Atakuletea juu yako magonjwa yote ya Misri
yale uliyoyaogopa, nayo yataambatana nawe.
61 Pia BWANA atakuletea kila aina ya ugonjwa
na maafa ambayo hayakuandikwa humu katika
kitabu hiki cha sheria, mpaka utakapokuwa
umeangamizwa.
62 Ninyi ambao mlikuwa wengi kama nyota
za angani mtaachwa wachache tu, kwa sababu
hamkumtii BWANA Mungu wenu.
63 Kama ilivyompendeza BWANA kuwafanya
ninyi mstawi na kuongezeka kwa idadi,
ndivyo itakavyompendeza kuwaharibu na
kuwaangamiza ninyi. Mtang'olewa kutoka
nchi mnayoiingia kuimiliki.

64 Kisha BWANA atawatawanya miongoni mwa
mataifa yote, kutoka mwisho mmoja wa dunia
hadi mwingine. Huko mtaabudu miungu
mingine, miungu ya miti na ya mawe, ambayo
ninyi wala baba zenu hamkuijua.
65 Miongoni mwa mataifa hayo hamtapata
raha wala mahali pa kupumzisha wayo wa mguu
wenu. Huko BWANA atawapa mahangaiko ya
mawazo, macho yaliyochoka kwa kungojea na

moyo uliokata tamaa.
66 Utaishi katika mahangaiko siku zote, ukiwa
umejaa hofu usiku na mchana, wala hutakuwa
kamwe na uhakika wa maisha yako.
67 Wakati wa asubuhi utasema hivi, “Laiti
ingekuwa jioni!” Jioni utasema, “Laiti ingekuwa
asubuhi,” kwa sababu ya hofu ile itakayojaza
moyo wako na vitu vile macho yako yatakavy-
oviona.
68 BWANA atawarudisha tena Misri kwa meli,
safari niliyosema kamwe hamngeenda tena.
Huko mtajiuza ninyi wenyewe kwa adui zenu
kama watumwa wa kiume na wa kike, lakini
hakuna yeyote atakayewanunua.

# 29

### *Kufanya Upya Agano*

1 Haya ndiyo maneno ya Agano BWANA aliy-
omwagiza Mose kufanya na Waisraeli huko
Moabu, kuwa nyongeza ya Agano alilofanya nao
huko Horebu.
2 Mose akawaita Waisraeli wote akawaambia:

Macho yenu yameona yale yote BWANA aliy-
ofanya kwa Mfalme Farao huko Misri, kwa
maafisa wake wote na kwa nchi yake yote.
3 Kwa macho yenu wenyewe mliona yale
majaribu makubwa, ishara zile za miujiza na
maajabu makubwa.
4 Lakini mpaka leo BWANA hajawapa akili
ya kuelewa au macho yanayoona au masikio
yanayosikia.

5 Kwa muda wa miaka arobaini niliyowaon-
goza jangwani, nguo zenu hazikuchakaa, wala
viatu miguuni mwenu.
6 Hamkula mkate na hamkunywa divai wala
kileo chochote. Nilifanya hivi ili mpate kujua
kuwa mimi ndimi BWANA Mungu wenu.

7 Wakati mlipofika mahali hapa, Sihoni
mfalme wa Heshboni na Ogu mfalme wa
Bashani walikuja kupigana dhidi yetu, lakini
tuliwashinda.
8 Tuliichukua nchi yao na kuwapa Wareubeni,
Wagadi na nusu ya kabila la Manase kama urithi
wao.
9 Fuateni kwa bidii masharti ya Agano hili,
ili kwamba mweze kustawi katika kila kitu
mnachofanya.
10 Ninyi nyote leo mnasimama mbele za BWANA
Mungu wenu; mkiwa viongozi na wakuu wenu,
wazee na maafisa wenu, na wanaume wengine
wote wa Israeli,
11 pamoja na watoto wenu, wake zenu na pia
wageni waishio katika kambi zenu wanaowapa-
sulia kuni na kuwachotea maji.
12 Mnasimama hapa ili kufanya Agano na
BWANA Mungu wenu, Agano ambalo Mungu
analifanya nanyi siku hii ya leo na kulitia
muhuri kwa kiapo,
13 kuwathibitisha ninyi siku hii ya leo kama
taifa lake, ili aweze kuwa Mungu wenu kama
alivyowaahidi na kama alivyowaapia baba zenu
Abrahamu, Isaki na Yakobo.
14 Ninafanya Agano hili pamoja na kiapo
chake, sio na ninyi tu

15 mnaosimama hapa na sisi leo mbele za
Bwana Mungu wetu, bali pia pamoja na wale
ambao hawapo hapa leo.
16 Ninyi wenyewe mnajua jinsi tulivyoishi
nchini Misri na jinsi tulivyopita katikati ya nchi
mpaka tukafika hapa.
17 Mliona miongoni mwao vinyago vyao vya
kuchukiza na sanamu za miti na mawe, za fedha
na dhahabu.
18 Hakikisheni kwamba hakuna mwanaume
au mwanamke, ukoo au kabila miongoni mwenu
leo ambalo moyo wake utamwacha Bwana
Mungu wetu, kwenda kuabudu miungu ya
mataifa hayo. Hakikisheni hakuna mzizi mion-
goni mwenu unaotoa sumu chungu ya namna
hii.
19 Wakati mtu wa namna hii asikiapo maneno
ya kiapo hiki, hujibariki mwenyewe na kisha hu-
fikiri, "Nitakuwa salama, hata kama nikiendelea
kuifuata njia yangu mwenyewe." Hili litaleta
maafa juu ya nchi iliyonyeshewa sawasawa na
nchi kame.
20 Bwana kamwe hatakuwa radhi kumsamehe,
ghadhabu na wivu wa Mungu vitawaka dhidi
ya mtu huyo. Laana zote zilizoandikwa katika
kitabu hiki zitamwangukia na Bwana atafuta
jina lake chini ya mbingu.
21 Bwana atamtwaa peke yake kutoka mak-
abila ya Israeli kwa maangamizo, kulingana
na laana zote za Agano zilizoandikwa kwenye
Kitabu hiki cha Sheria.
22 Watoto wako watakaofuata baada yako
katika vizazi vya baadaye na wageni ambao
watakuja kutoka nchi za mbali, wataona maafa,

yaliyoipata nchi na magonjwa ambayo Bwana
aliyaleta juu yake.
23 Nchi yote itakuwa jaa linaloungua la
chumvi na kiberiti: hakutakuwa kilichopandwa,
hakutakuwa kinachochipua, wala hakutakuwa
mimea inayoota juu yake. Itakuwa kama
maangamizo ya Sodoma na Gomora, Adma
na Seboimu, ambazo Bwana aliangamiza kwa
hasira kali.
24 Mataifa yote yatauliza: “Kwa nini Bwana
amefanya hivi juu ya nchi hii? Kwa nini hasira
hii kali ikawaka?”
25 Na jibu litakuwa: “Ni kwa sababu watu
hawa waliacha Agano la Bwana, Mungu wa baba
zao, Agano alilofanya nao wakati alipowatoa
katika nchi ya Misri.
26 Walienda zao na kuabudu miungu mingine
na kuisujudia, miungu wasioijua, miungu am-
bayo Mungu hakuwapa.
27 Kwa hiyo hasira ya Bwana ikawaka dhidi
ya nchi hii, hivyo Mungu akaleta juu yake laana
zote zilizoandikwa katika kitabu hiki.
28 Katika hasira kali na katika ghadhabu kuu
Bwana aliwang’oa kutoka nchi yao na kuwa-
sukumia katika nchi nyingine, kama ilivyo sasa.”
29 Mambo ya siri ni ya Bwana Mungu wetu,
bali yaliyofunuliwa ni yetu na watoto wetu
milele, ili tuweze kuyafanya maneno yote ya
sheria hii.

# 30

*Mafanikio Baada Ya Kumgeukia Bwana*

1 Wakati baraka hizi zote pamoja na laana nilizoziweka mbele yako zitakapokujia, nawe ukazitafakari moyoni popote BWANA Mungu wako atakapokutawanya miongoni mwa mataifa,
2 hapo wewe na watoto wako mtakapomrudia BWANA Mungu wako, na kumtii kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote kulingana na kila kitu ninachokuamuru leo,
3 ndipo BWANA Mungu wako atakapokurudisha kutoka utumwani na kukuhurumia, naye atakukusanya tena kutoka mataifa yote kule alikutawanya.
4 Hata kama umefukuziwa katika nchi ya mbali kiasi gani chini ya mbingu, kutoka huko BWANA Mungu wako atakukusanya na kukurudisha.
5 Yeye BWANA atakurudisha katika nchi iliyokuwa mali ya baba zako, nawe utaimiliki. Naye atakufanya ufanikiwe sana na kukuzidisha kwa idadi kuliko baba zako.
6 BWANA Mungu wako ataitahiri mioyo yenu na mioyo ya wazao wenu ili mweze kumpenda kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote ukaishi.
7 BWANA Mungu wako ataweka laana hizi zote juu ya adui zako ambao wanakuchukia na kukutesa.
8 Utamtii tena BWANA na kuzishika amri zake zote ninazokupa leo.
9 Ndipo BWANA Mungu wako atakapokufanikisha sana katika kazi zote za mikono yako na katika uzao wa tumbo lako, wadogo wa mifugo yako na mazao ya nchi yako. BWANA atakufurahia tena na kukufanikisha, kama alivyowafu-

rahia baba zako,
10 kama ukimtii BWANA Mungu wako, na
kuzishika amri zake na maagizo yake ambayo
yameandikwa katika Kitabu hiki cha Sheria, na
kumgeukia BWANA Mungu wako kwa moyo wako
wote na kwa roho yako yote.

### *Uzima Na Mauti*

11 Ninachokuagiza leo sio kigumu sana kwako
au usichokiweza.
12 Hakiko juu mbinguni, ili uulize, “Ni
nani atakayepanda mbinguni kukileta na kutu-
tangazia ili tuweze kutii?”
13 Wala hakiko ng’ambo ya bahari, ili uulize,
“Ni nani atakayevuka bahari kwenda ku-
kichukua na kututangazia ili tupate kutii?”
14 La hasha! Lile neno liko karibu sana nawe;
liko kinywani mwako na ndani ya moyo wako ili
uweze kulitii.
15 Tazama, naweka mbele yako leo uzima na
mafanikio, mauti na maangamizo.
16 Ninakuamuru leo kwamba umpende BWANA
Mungu wako, utembee katika njia zake, na
kutunza maagizo yake, amri na sheria zake;
ndipo utakapoishi na kuongezeka, naye BWANA
Mungu wako atakubariki katika nchi unayoingia
kuimiliki.
17 Lakini kama moyo wako ukigeukia mbali
ukawa huna utii, kama umevutwa kuisujudia
miungu mingine na kuiabudu,
18 nakutangazia leo hii kwamba hakika
utaangamizwa. Hutaishi maisha marefu katika
nchi unayovuka Yordani kuiingia na kuimiliki.

19 Leo ninaziita mbingu na nchi kama
mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka mbele
yako uzima na mauti, baraka na laana. Basi sasa
chagueni uzima, ili wewe na watoto wako mpate
kuishi,
20 na ili upate kumpenda BWANA Mungu wako,
uisikilize sauti yake na kuambatana naye. Kwa
kuwa BWANA ndiye uzima wako, na atakupa
wingi wa siku ili upate kuishi katika nchi
aliyoapa kuwapa baba zako Abrahamu, Isaki na
Yakobo.

# 31

### *Yoshua Kutawala Baada Ya Mose*
### *(Hesabu 27:12-23)*

1 Kisha Mose akaenda akasema maneno haya
kwa Waisraeli wote:
2 "Sasa nina miaka mia moja na ishirini nami
siwezi tena kuwaongoza. BWANA ameniambia,
'Hutavuka Yordani.'
3 BWANA Mungu wenu, yeye mwenyewe
atavuka mbele yenu. Ataangamiza mataifa
haya mbele yenu, nanyi mtaimiliki nchi yao.
Pia Yoshua atavuka mbele yenu, kama BWANA
alivyosema.
4 Naye BWANA atawafanyia watu hao kile
alichowafanyia Sihoni na Ogu, wafalme wa
Waamori, ambao aliwaangamiza pamoja na nchi
yao.
5 BWANA atawakabidhi kwenu, nanyi lazima
mwatendee yale yote niliyowaamuru.
6 Kuweni imara na moyo wa ushujaa. Msio-
gope wala msifadhaike kwa sababu yao, kwa

kuwa BWANA Mungu wenu anakwenda pamoja nanyi; kamwe hatawaacha wala hatawatupa ninyi.”

7 Kisha Mose akamwita Yoshua na akamwambia mbele ya Israeli wote, “Uwe imara na moyo wa ushujaa, kwa kuwa ni lazima uende na watu hawa katika nchi ile BWANA aliyowaapia baba zao kuwapa, nawe ni lazima uwagawie kama urithi wao.

8 BWANA mwenyewe atakutangulia naye atakuwa pamoja nawe; kamwe hatakuacha wala hatakutupa. Usiogope, wala usifadhaike.”

### *Kusoma Sheria*

9 Kwa hiyo Mose akaandika sheria hii na kuwapa makuhani, wana wa Lawi, waliochukua Sanduku la Agano la BWANA na wazee wote wa Israeli.

10 Kisha Mose akawaamuru, akasema: “Mwishoni mwa kila miaka saba, katika mwaka wa kufuta madeni, wakati wa Sikukuu ya Vibanda,

11 Waisraeli wote wanapokuja mbele za BWANA Mungu wenu mahali atakapopachagua, utasoma sheria hii mbele yao masikioni mwao.

12 Kusanya watu wote, wanaume, wanawake, watoto na wageni wanaoishi katika miji yenu, ili waweze kusikia na kujifunza kumcha BWANA Mungu wenu na kufuata kwa bidii maneno yote ya sheria hii.

13 Watoto wao, ambao hawaijui sheria hii, lazima waisikie na kujifunza kumcha BWANA Mungu wenu kwa muda mtakaoishi katika nchi mnayovuka Yordani kuimiliki.”

## *Kuasi Kwa Waisraeli Kunatabiriwa*

14 BWANA akamwambia Mose, “Sasa siku ya
kifo chako imekaribia. Mwite Yoshua, mkaji-
hudhurishe katika Hema la Kukutania, mahali
nitakapompa maagizo ya kazi.” Kwa hiyo Mose
na Yoshua wakaja na kujihudhurisha kwenye
Hema la Kukutania.
15 Kisha BWANA akatokea katika Hema katika
nguzo ya wingu, nalo wingu likasimama juu ya
ingilio la Hema.
16 Kisha BWANA akamwambia Mose: “Un-
akwenda kupumzika na baba zako, nao watu
hawa hivi karibuni watazini na miungu migeni
ya nchi wanayoingia. Wataniacha na kuvunja
Agano nililofanya nao.
17 Siku hiyo nitawakasirikia na kuwaacha;
nitawaficha uso wangu, nao wataangamizwa.
Maafa mengi na shida nyingi zitakuja juu
yao, nao siku hiyo watauliza, ‘Je, maafa haya
hayakuja juu yetu kwa sababu Mungu wetu
hayuko pamoja nasi?’
18 Nami hakika nitauficha uso wangu siku hiyo
kwa sababu ya maovu yao yote kwa kugeukia
miungu mingine.

19 “Sasa ujiandikie wimbo huu,* uwafundishe
Waisraeli na uwaamuru wauimbe, ili upate
kuwa ushahidi wangu dhidi yao.
20 Nitakapokwisha kuwaingiza katika nchi
itiririkayo maziwa na asali, nchi niliyowaahidi
baba zao kwa kiapo, nao watakapokula
wakashiba na kufanikiwa, watageukia miungu

---

* **31:19** Wimbo huu hapa ina maana wimbo wa Mose.

mingine na kuiabudu, wakinikataa mimi na kuvunja Agano langu.

21 Maafa na shida zitakapokuja juu yao, wimbo huu utashuhudia dhidi yao, kwa sababu hautasahauliwa na wazao wao. Ninajua lile wanaloandaa kufanya, hata kabla sijawaingiza katika nchi niliyowaahidi kwa kiapo.”

22 Hivyo Mose akaandika wimbo huu siku ile na akawafundisha Waisraeli.

23 BWANA akampa Yoshua mwana wa Nuni agizo hili: “Uwe hodari na shujaa, kwa kuwa utawaleta Waisraeli katika nchi niliyowaahidi kwa kiapo, nami mwenyewe nitakuwa pamoja nawe.”

24 Baada ya Mose kumaliza kuandika kwenye kitabu maneno ya sheria hii kutoka mwanzo hadi mwisho,

25 akawapa Walawi wale waliolibeba Sanduku la Agano la BWANA agizo hili, akawaambia:

26 “Chukueni Kitabu hiki cha Sheria mkakiweke kando ya Sanduku la Agano la BWANA Mungu wenu. Hapo ndipo kitakapokaa kama shahidi dhidi yenu.

27 Kwa kuwa ninajua jinsi mlivyo waasi na mlivyo na shingo ngumu. Kama mmekuwa mkiasi dhidi ya BWANA nikiwa bado niko hai na nikiwa pamoja nanyi, mtaasi mara ngapi baada ya kufa kwangu!

28 Kusanyeni mbele yangu wazee wote wa makabila yenu na maafisa wenu wote, ili nipate kusema maneno haya masikioni mwao na kuziita mbingu na nchi ili kushuhudia dhidi yao.

29 Kwa kuwa ninajua baada ya kifo changu
hakika mtakuwa waovu kabisa na kugeuka kutoka njia niliyowaamuru ninyi. Katika siku zijazo, maafa yatawapata kwa sababu mtafanya maovu mbele ya macho ya BWANA, na kuchochea hasira yake kwa yale mikono yenu itakayokuwa imefanya."

### *Wimbo Wa Mose*

30 Mose akayasoma maneno ya wimbo huu
kutoka mwanzo hadi mwisho katika masikio ya kusanyiko lote la Israeli:

## 32

1 Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitasema;
sikia, ee nchi, maneno ya kinywa changu.
2 Mafundisho yangu na yanyeshe kama mvua,
na maneno yangu na yashuke kama umande,
kama manyunyu juu ya majani mabichi,
kama mvua tele juu ya mimea myororo.

3 Nitalitangaza jina la BWANA.
Naam, sifuni ukuu wa Mungu wetu!
4 Yeye ni Mwamba, kazi zake ni kamilifu,
njia zake zote ni haki.
Mungu mwaminifu ambaye hakosei,
yeye ni mnyofu na mwenye haki.

5 Wamefanya mambo ya upotovu mbele zake;
kwa aibu yao, wao si watoto wake tena,
lakini ni kizazi kilicho kiovu na kilichopotoka.
6 Je, hii ndiyo njia ya kumlipa BWANA,

enyi watu wajinga na wasio na busara?
Je, yeye siye Baba yenu, Muumba wenu,
aliyewafanya ninyi na kuwaumba?

7 Kumbuka siku za kale;
tafakari vizazi vya zamani vilivyopita.
Uliza baba yako, naye atakuambia,
wazee wako, nao watakueleza.
8 Aliye Juu Sana alipowapa mataifa urithi wao,
alipogawanya wanadamu wote,
aliweka mipaka kwa ajili ya mataifa
sawasawa na hesabu ya wana wa Israeli.
9 Kwa kuwa fungu la BWANA ni watu wake,
Yakobo kura yake ya urithi.

10 Katika nchi ya jangwa alimkuta,
katika nyika tupu ivumayo upepo.
Alimhifadhi na kumtunza;
akamlinda kama mboni ya jicho lake,
11 kama tai avurugaye kiota chake,
na kurukaruka juu ya makinda yake,
ambaye hutanda mabawa yake kuwadaka,
na huwachukua kwenye mabawa yake.
12 BWANA peke yake alimwongoza;
hakuwepo mungu mgeni pamoja naye.

13 Akamfanya apande sehemu zilizoinuka za nchi,
akamlisha kwa mavuno ya mashamba.
Akamlea kwa asali toka mwambani,
na kwa mafuta kutoka mwamba mgumu,
14 kwa jibini na maziwa kutoka makundi ya ng'ombe

na kutoka makundi ya mbuzi,
kwa mafuta ya wana-kondoo na mbuzi,
kwa kondoo dume wazuri wa Bashani,
na kwa ngano nzuri.
Ukanywa damu ya zabibu inayotoa povu.

15 Yeshuruni* alinenepa na kupiga teke;
alikuwa na chakula tele,
akawa mzito na akapendeza sana.
Akamwacha Mungu aliyemuumba,
na kumkataa Mwamba Mwokozi wake.
16 Wakamfanya Mungu kuwa na wivu kwa miungu yao migeni,
na kumkasirisha kwa sanamu zao
za machukizo.
17 Wakatoa dhabihu kwa pepo, ambao si Mungu:
miungu wasiyoijua,
miungu iliyojitokeza siku za karibuni,
miungu ambayo baba zenu hawakuiogopa.
18 Mkamwacha Mwamba, aliyewazaa ninyi;
mkamsahau Mungu aliyewazaa.

19 Bwana akaona hili, akawakataa,
kwa sababu alikasirishwa
na wanawe na binti zake.
20 Akasema, "Nitawaficha uso wangu,
nami nione mwisho wao utakuwa nini,
kwa kuwa wao ni kizazi kilichopotoka,
watoto ambao si waaminifu.
21 Wamenifanya niwe na wivu
kwa kile ambacho si mungu,
na kunikasirisha kwa sanamu zao

* **32:15** Yeshuruni maana yake ni Yeye aliye mnyofu, yaani Israeli (ona pia Kum 33:26; Isa 44:2).

zisizokuwa na thamani.
Nitawafanya wawaonee wivu wale ambao si taifa.
Nitawafanya wakasirishwe
na taifa lile lisilo na ufahamu.
22 Kwa maana moto umewashwa kwa hasira yangu,
ule uwakao hadi kwenye vina vya mauti.
Utateketeza dunia pamoja na mazao yake,
na kuwasha moto katika misingi ya milima.

23 “Nitalundika majanga juu yao
na kutumia mishale yangu dhidi yao.
24 Nitatuma njaa kali dhidi yao maradhi mabaya,
yateketezayo na tauni ya kufisha;
nitawapelekea meno makali ya wanyama mwitu,
na sumu ya nyoka wale watambaao mavumbini.
25 Barabarani upanga utawakosesha watoto;
nyumbani mwao hofu itatawala.
Vijana wao wa kiume na wa kike wataangamia,
pia watoto wachanga na wazee wenye mvi.
26 Nilisema ningewatawanya
na kufuta kumbukumbu lao
katika mwanadamu.
27 Lakini nilihofia dhihaka za adui,
adui asije akashindwa kuelewa,
na kusema, ‘Mikono yetu imeshinda;
BWANA hakufanya yote haya.’ ”

28 Wao ni taifa lisilo na akili,
hakuna busara ndani yao.
29 Laiti wangekuwa na hekima wangefahamu hili,

na kutambua mwisho wao utakuwa aje!
30 Mtu mmoja angewezaje kufukuza elfu moja,
au wawili kufukuza elfu kumi,
kama si kwamba Mwamba wao amewauza,
kama si kwamba BWANA amewaacha?
31 Kwa kuwa mwamba wao si kama Mwamba wetu,
sawasawa na vile adui zetu wanavyokiri.
32 Mzabibu wao unatoka kwenye mzabibu wa Sodoma,
na kutoka kwenye mashamba ya Gomora.
Zabibu zake zimejaa sumu,
na vishada vyake vimejaa uchungu.
33 Mvinyo wao ni sumu ya nyoka,
sumu yenye kufisha ya swila.

34 "Je, hili sikuliweka akiba
na kulifungia kwenye vyumba vyangu vya hazina?
35 Ni juu yangu kulipiza kisasi; nitalipiza.
Wakati utakapowadia, mguu wao utateleza;
siku yao ya maafa ni karibu,
na maangamizo yao yanawajia haraka."

36 BWANA atawahukumu watu wake,
na kuwahurumia watumishi wake
atakapoona nguvu zao zimekwisha
wala hakuna yeyote aliyebaki,
mtumwa au aliye huru.
37 Atasema: "Sasa iko wapi miungu yao,
mwamba walioukimbilia,
38 miungu wale waliokula mafuta ya dhabihu zao
na kunywa mvinyo wa sadaka zao za vinywaji?

Wainuke basi, wawasaidie!
Wawapeni basi ulinzi!

39 “Tazama basi, Mimi mwenyewe, Mimi Ndiye!
Hakuna mungu mwingine ila Mimi.

Mimi ninaua na Mimi ninafufua,
Mimi nimejeruhi na Mimi nitaponya,
wala hakuna awezaye kuokoa kutoka mkononi mwangu.

40 Ninainua mkono wangu kuelekea mbinguni na kusema:
Hakika kama niishivyo milele,

41 wakati ninapounoa upanga wangu unaometameta
na mkono wangu unapoushika ili kutoa hukumu,

nitalipiza kisasi juu ya adui zangu
na kuwalipiza wale wanaonichukia.

42 Nitailevya mishale yangu kwa damu,
wakati upanga wangu ukitafuna nyama:

damu ya waliochinjwa pamoja na mateka,
vichwa vya viongozi wa adui.”

43 Furahini, enyi mataifa, pamoja na watu wake,
kwa kuwa atailipiza damu ya watumishi wake,

atalipiza kisasi juu ya adui zake
na kufanya upatanisho
kwa ajili ya nchi na watu wake.

44 Mose na Yoshua† mwana wa Nuni wakaja,
wakanena maneno yote ya wimbo watu wakiwa
wanasikia.
45 Mose alipomaliza kuyasoma maneno haya
yote kwa Israeli wote,
46 akawaambia, “Yawekeni moyoni maneno
yote ambayo nimewatangazia kwa makini siku
hii ya leo, ili kwamba mpate kuwaagiza watoto
wenu wayatii kwa bidii maneno yote ya sheria
hii.
47 Siyo maneno matupu tu kwenu, bali ni
uzima wenu. Kwa hayo mtaishi maisha marefu
katika nchi mnayovuka Yordani kuimiliki.”

### *Mose Aelezwa Kuhusu Kifo Chake*

48 Siku hiyo hiyo BWANA akamwambia Mose,
49 “Kwea katika mapangano ya Mlima
Abarimu hadi kilima cha Nebo kilichoko Moabu,
ng’ambo ya Yeriko, na uitazame Kanaani, nchi
ninayowapa Waisraeli kama milki yao wenyewe.
50 Utafia kwenye mlima huo unaokwea na
kukusanyika pamoja na watu wako, kama ndugu
yako Aroni alivyofia juu ya Mlima Hori naye
akakusanyika kwa watu wake.
51 Hii ni kwa sababu ninyi wawili mlivunja
uaminifu nami mbele ya Waisraeli kwenye maji
ya Meriba-Kadeshi katika Jangwa la Sini, na kwa
sababu hamkuuinua utakatifu wangu miongoni
mwa Waisraeli.
52 Kwa hiyo, utaiona tu nchi kwa mbali; wewe
hutaingia nchi ninayowapa watu wa Israeli.”

---

† **32:44** Yoshua, yaani Yehoshea kwa Kiebrania, maana yake ni Yehova ni Mwokozi.

# 33

## *Mose Anayabariki Makabila*

1 Hii ndiyo baraka Mose mtu wa Mungu aliy-
otamka kwa Waisraeli kabla ya kifo chake.
2 Alisema:
"Bwana alikuja kutoka Mlima Sinai,
akachomoza kama jua juu yao
kutoka Mlima Seiri,
akaangaza kutoka Mlima Parani.
Alikuja pamoja na watakatifu makumi elfu
kutoka kusini,
kutoka materemko ya mlima wake.
3 Hakika ni wewe ambaye huwapenda watu,
watakatifu wako wote wamo mkononi
mwako.
Miguuni pako wote wanasujudu
na kutoka kwako wanapokea mafundisho,
4 sheria ile Mose aliyotupa sisi,
tulio milki ya kusanyiko la Yakobo.
5 Alikuwa mfalme juu ya Yeshuruni*
wakati viongozi wa watu walipokusanyika,
pamoja na makabila ya Israeli.

6 "Reubeni na aishi, asife,
wala watu wake wasiwe wachache."
7 Akasema hili kuhusu Yuda:
"Ee Bwana, sikia kilio cha Yuda,
mlete kwa watu wake.
Kwa mikono yake mwenyewe hujitetea.
Naam, uwe msaada wake
dhidi ya adui zake!"
8 Kuhusu Lawi alisema:

* **33:5** Yeshuruni maana yake ni Yeye aliye mnyofu, yaani Israeli.

"Thumimu yako na Urimu[†] yako ulimpa,
mtu yule uliyemfadhili.
Ulimjaribu huko Masa
na kushindana naye
kwenye maji ya Meriba.
9 Alinena hivi kuhusu baba yake na mama yake,
'Mimi siwahitaji kamwe.'
Akawasahau jamaa zake,
asiwatambue hata watoto wake,
lakini akaliangalia neno lako
na kulilinda Agano lako.
10 Humfundisha Yakobo mausia yako
na Israeli sheria yako.
Hufukiza uvumba mbele zako
na sadaka nzima za kuteketezwa
juu ya madhabahu yako.
11 Ee BWANA, bariki ustadi wake wote,
nawe upendezwe na kazi ya mikono yake.
Vipige viuno vya wale wainukao dhidi yake;
wapige adui zake hata wasiinuke tena."
12 Kuhusu Benyamini akasema:
"Mwache mpenzi wa BWANA
apumzike salama kwake,
kwa maana humkinga mchana kutwa,
na yule BWANA ampendaye
hupumzika kati ya mabega yake."
13 Kuhusu Yosefu akasema:
"BWANA na aibariki nchi yake
kwa umande wa thamani
kutoka mbinguni juu,

---

[†] **33:8** Thumimu na Urimu maana yake Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha kifuani cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.

na vilindi vya maji
vilivyotulia chini;
14 pamoja na vitu vilivyo bora sana
viletwavyo na jua,
na vitu vizuri sana vinavyoweza
kutolewa na mwezi;
15 pamoja na zawadi bora sana
za milima ya zamani
na kwa wingi wa baraka
za vilima vya milele;
16 pamoja na baraka nzuri mno
za ardhi na ukamilifu wake,
na upendeleo wake yeye
aliyeishi kwenye kichaka
kilichokuwa kinawaka moto.
Hivi vyote na vikae juu ya kichwa cha Yosefu,
juu ya paji la uso la aliye mkuu
miongoni mwa ndugu zake.
17 Katika fahari yeye ni kama fahali mzaliwa wa
kwanza;
pembe zake ni pembe za nyati,
na kwa pembe hizo atapiga mataifa,
hata yaliyo miisho ya dunia.
Hivyo ndivyo yalivyo makumi elfu ya Efraimu;
hivyo ndivyo yalivyo maelfu ya Manase.”
18 Kuhusu Zabuloni akasema:
“Shangilia, Zabuloni, wakati wa kutoka nje,
nawe Isakari, katika mahema yako.
19 Watawaita mataifa kwenye mlima,
na huko mtatoa dhabihu za haki;
watajifurahisha kwa wingi uliojaza bahari,
kwa hazina zilizofichwa mchangani.”
20 Kuhusu Gadi akasema:

"Atabarikiwa yeye aongezaye milki ya Gadi!
Gadi huishi huko kama simba,
akirarua kwenye mkono au kichwa.
21 Alijichagulia nchi nzuri kuliko zote
kwa ajili yake mwenyewe;
fungu la kiongozi lilikuwa limehifadhiwa
kwa ajili yake.
Viongozi wa watu walipokusanyika,
alitimiza haki ya mapenzi ya BWANA,
na hukumu zake kuhusu Israeli."
22 Kuhusu Dani akasema:
"Dani ni mwana simba,
akiruka kutoka Bashani."
23 Kuhusu Naftali akasema:
"Naftali amejaa tele upendeleo wa BWANA,
naye amejaa baraka yake;
atarithi magharibi na kusini."
24 Kuhusu Asheri akasema:
"Aliyebarikiwa zaidi sana katika wana ni Asheri;
yeye na apate upendeleo kwa ndugu zake,
yeye na anawe miguu yake kwenye mafuta.
25 Makomeo ya malango yako yawe chuma na shaba,
nazo nguvu zako zitakuwa sawa na siku zako.

26 "Hakuna mwingine kama Mungu wa Yeshuruni,
ambaye hupanda juu ya mbingu ili akusaidie,
na juu ya mawingu katika utukufu wake.
27 Mungu wa milele ni kimbilio lako,
na chini kuna mikono ya milele.
Atamfukuza adui yako mbele yako,

akisema, 'Mwangamize yeye!'
28 Hivyo Israeli ataishi salama peke yake.
Mzao wa Yakobo ni salama
katika nchi ya nafaka na divai mpya,
mahali ambapo mbingu
hudondosha umande.
29 Ee Israeli, wewe umebarikiwa!
Ni nani kama wewe,
taifa lililookolewa na BWANA?
Yeye ni ngao yako na msaada wako,
na upanga wako uliotukuka.
Adui zako watatetemeka mbele yako,
nawe utapakanyaga
mahali pao pa juu."‡

# 34

## *Kifo Cha Mose*

1 Kisha Mose akaupanda mlima Nebo kutoka
tambarare za Moabu mpaka kilele cha Pisga,
ng'ambo ya Yeriko. Huko BWANA akamwonyesha
nchi yote: kutoka Gileadi mpaka Dani,
2 Naftali yote, nchi ya Efraimu na Manase, nchi
yote ya Yuda mpaka bahari ya magharibi,*
3 Negebu na nchi yote kuanzia Bonde la Yeriko,
Mji wa Mitende, hadi Soari.
4 Kisha BWANA akamwambia, "Hii ndiyo nchi
niliyomwahidi Abrahamu na Isaki na Yakobo
kwa kiapo niliposema, 'Nitawapa wazao wako.'
Nimekuruhusu uione kwa macho yako, lakini
hutavuka kuingia."

‡ **33:29** Utapakanyaga mahali pao pa juu maana yake mtakanyaga juu ya miili yao. * **34:2** Yaani Bahari ya Mediterania.

5 Naye Mose mtumishi wa BWANA akafa huko
Moabu, kama BWANA alivyokuwa amesema.
6 Mungu akamzika huko Moabu, katika bonde
mkabala na Beth-Peori, lakini hakuna ajuaye
kaburi lake lilipo mpaka leo.
7 Mose alikuwa na umri wa miaka mia moja na
ishirini alipofariki; hata hivyo nguvu ya macho
yake haikufifia wala mwili wake haukudhoofika.
8 Waisraeli wakaomboleza kwa ajili ya Mose
kwenye tambarare za Moabu kwa siku the-
lathini, mpaka wakati wa kulia na kuomboleza
ulipopita.
9 Basi Yoshua mwana wa Nuni alijazwa roho
ya hekima kwa sababu Mose alikuwa ameweka
mikono yake juu yake. Kwa hiyo Wais-
raeli wakamsikiliza na wakafanya yale ambayo
BWANA alikuwa amemwagiza Mose.
10 Tangu wakati huo, katika Israeli hajainuka
nabii mwingine kama Mose, ambaye BWANA
alimjua uso kwa uso,
11 aliyetenda ishara zote zile za miujiza na
maajabu ambayo BWANA alimtuma kuyatenda
huko Misri, yaani kwa Farao na maafisa wake
wote na nchi yake yote.
12 Kwa kuwa hakuna mtu yeyote aliyewahi
kuonyesha nguvu nyingi ama kutenda matendo
ya kutisha ambayo Mose aliwahi kuyafanya
mbele ya Israeli yote.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
## Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™ (Bible)

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.
You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

- You include the above copyright and source information.
- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.
Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files dated 31 Aug 2023
9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462